UKIUKAJI WA KANUNI YA KUFUTA MABANO KATIKA UUNDAJI WA NOMINO AMBATANI ZA KISWAHILI: MTAZAMO WA MOFOLOJIA LEKSIA

MOFART ONYONI AYIEGA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

FEBRUARI, 2022

UNGAMO NA IDHINI

Tasnifu hii ni yangu na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi..... Tarehe 11/02/2022

Mofart Onyoni Ayiega

C50/28000/2018

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ruhusa yangu kama msimamizi aliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Dkt. Leonard Mwita Chacha

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi..... Tarehe 11/02/2022

TABARUKU

Utafiti huu nautabaruku kwa wazazi wangu wapendwa James Ayiega Ongoya na Florence Moragwa Ongoya kwa kugharamia masomo yangu na kunitia shime ya kuendelea na masomo hadi upeoni. Vilevile, nautabaruku utafiti huu kwa kaka yangu Omiko, na dada zangu Bochere, Kwamboka, Moraa na Sarange ambao wamekuwa mhimili mkuu wa kunitia moyo katika safari hii ya kiusomi wakati nilitaka kujiondoa. Mungu awape maisha marefu kwa ukarimu wenu.

SHUKRANI

Namshukuru Maulana kwa kunipa uwezo, neema na busara ya namna ya kufanya kazi hii. Shukrani za dhati pia kwa msimamizi wangu Dkt. Leonard Chacha Mwita ambaye hakuchoka kusoma kazi yangu na kunitia shime wakati nilipoonekana kukata tamaa. Asante sana daktari kwa kutembea nami katika safari ambayo imekuwa na panda shuka tele. Ni mengi ya kukushukuru na huenda nikapungukiwa na maneno ya kueleza jinsi ulivyonifaa ila nakuombea amani maishani na Maulana akupe maghufira yako katika shughuli zako za kila siku. Inshallah! Pia namshukuru Dkt. David Kung'u Kihara kwa ushauri na kunipa imani ya kukamilisha safari hii, ambayo hatimaye imefika tamati. Nawashukuru kwa dhati wahadhiri walionifunza: Profesa Kitula King'ei, Dkt. Richard Wafula, Dkt. Pamela Ngugi, Dkt. Timothy Arege, Dkt. Jacktone Onyango, Dkt. Edwin Masinde, Dkt. Boniface Ngugi, na Dkt. Eunice Nyamasyo. Kutangamana nanyi darasani na hata nje ya darasa kulinipa kariha ya kuendelea na hii safari ya kiusomi. Vilevile, sitawasahau waktubi wa maktaba ya idara ya Kiswahili na maktaba kuu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunipa usaidizi wakati nilipokuwa nikifanya utafiti huu. Mungu awabariki!

Ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu wa umahiri: Simon, Imelda, Annbridgit, Sato, Evans, Fidelis, Jemimah na Immaculate kwa kushirikiana nami katika safari hii. Uwepo wenu ulichangia sana katika ufanisi wa masomo yangu hasa vipindi vya darasani. Nawatakia bahati njema maishani na Rabuka awe nanyi siku zote. Mwisho kabisa nashukuru uongozi wa Chuo cha Kenyatta kwa kunipa nafasi ya kusomea chuoni humo, na galacha wa idara ya Kiswahili waliotenga muda wao kuisoma kazi hii, na kutoa mapendekezo yaliyofanikisha kuboresha kazi hii kuwa sawa. Rabii awabariki maradufu.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili. Nomino ambatani ni mofu changamano (Mgullu; 1999). Kanuni ya Kufuta Mabano huonyesha hatua zinazotumiwa kuunda neno sahihi kwa kutumia viambajengo. Mabano katika kanuni hii hudhihirisha mipaka na hufutwa kuashiria kuwa sheria za uundaji wa maneno hazina ufikiaji wa umbo la neno linalotokana na ngazi za awali. Uchunguzi huu ulifanywa baada ya kubaini kuwa baadhi ya nomino ambatani za Kiswahili hukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano hasa pale ambapo mabadiliko hutokea katikati mwa neno baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa. Data ya uchunguzi huu ilikusanywa kutoka kwenye *Kamusi Kuu ya Kiswahili (*2015) ambapo nomino ambatani thelathini zinazoghairi thelathini zisizoghairi Kanuni ya Kufuta Mabano mtawalia zilitumika. Nomino hizi zilichaguliwa kwa kuzingatia uwepo wa sifa za ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano (KKM). Malengo ya uchunguzi huu yalikuwa ni: kudhihirisha nomino ambatani za Kiswahili zinazoghairi KKM ya Mofolojia Leksia (ML). Kudhihirisha maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM ya Mofolojia Leksia, kubainisha sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki, na kueleza mchango wa ukiukaji wa KKM ya Mofolojia Leksia kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Ili kufanikisha utafiti huu, nadharia ya Mofolojia Leksia iliyoanzishwa na Kiparsky (1982) na kufafanuliwa zaidi na Katamba & Stonham (2019): Kanuni ya Kufuta Mabano na Kanuni ya Mzunguko Kamili iliongoza uchunguzi huu. Data ya uchunguzi huu ilikusanywa maktabani. Baadhi ya makala zilizotumika katika uchunguzi huu ni tasnifu, makala yaliyosakurwa mtandaoni na majarida. Usampulishaji kimakusudi uliongoza uchunguzi huu ili kufikia maneno husika ya nomino ambatani yaliyodhihirisha ukiukaji wa KKM. Matokeo ya uchunguzi huu yamedhihirisha kuwa ukiukaj wa Kanuni ya Kufuta Mabano husababishwa na mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana na mofu ya kwanza, na muktadha wa matumizi ya nomino ambatani katika mawasiliano ya kila siku. Utafiti huu ni nafasi bora ya kuchangia isimu hasa kupitia kufahamu na kufafanua mwambatano katika Kiswahili, kuwahami waundakamusi za Kiswahili na maarifa, kukuza mofolojia ya Kiswahili na kuchochea uchunguzi zaidi.

ABSTRACT

This research intended to investigate violation of the bracket erasure rule in the formation of compound nouns of Kiswahili. Compound nouns are complex morphs (Mgullu; 1999). The bracket erasure rule shows the procedure of constructing a full word using components. Brackets in this rule reveal that boundaries are deleted after the word is created. This study was conducted after discovering some of the Kiswahili compound nouns violate the bracket erasure rule, especially where changes occur in the middle of a word after various constituents have been combined. In this study, we collected data from the *Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015)* in which thirty violating compound nouns, and thirty compound nouns that do not violate the bracket erasure rule was used as the primary data. The objectives of this research include; identifying Kiswahili compound nouns that violate the bracket erasure rule in Lexical Morphology. Revealing the forms of Kiswahili compound nouns that violate the bracket erasure rule in Lexical Morphology, examining why some compound nouns violate the bracket erasure rule while others do not violate the rule, and to explain the contribution of the violation of bracket erasure rule of Lexical Morphology to Kiswahili lexicographers. The study conducted was guided by two tenets of Lexical Morphology theory that was invented by Kiparsky (1982) and developed by Katamba & Stonham (2019) : Bracket Erasure Rule and Strict Cyclicity Rule with relevant data being collected in the library to shed more light on the research. Some of the sources that were used in this research are theses, online articles, and journals. This study was guided by a purposive sampling technique to achieve relevant compound nouns with the required features. The findings of this study have revealed that the violation of the brackets erasure rule is caused by the second morph of the compound nouns being seen by the first morph, and the contextual use of these nouns in the daily communication. This research is an opportunity to contribute to linguistics, especially through understanding and explaining the techniques of compounding of nouns in the Kiswahili language; that is, to equip Kiswahili lexicographers with skills, develop Kiswahili morphology, and trigger further investigations.

UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

Hali ya kupakana:	Kanuni ambayo huzuia kuangalia historia nzima ya neno ila katika muktadha wa mofu moja.
Kanuni:	Utaratibu wa kuzingatiwa katika lugha husika.
Kufuta:	Hali ya kuondoa utaratibu uliopo.
Mkataba wa kufuta mabano:	Kanuni ambayo hairuhusu urejeleaji nyuma baada ya mabano yamefutwa.
Mofimu:	Kipashio cha lugha ambacho huchukua kiambishi cha wingi kubadili maana ya neno.
Mofu:	Umbo la neno linalowakilisha mofimu na hudhihirika kiothografia.
Mwambatano:	Mbinu ya kuweka maneno mawili pamoja ili kuunda neno jipya.
Nomino ambatani:	Nomino yenye maneno mawili ambayo huunganishwa ili kuunda istilahi mpya.
Uambishaji:	Utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi.
Ukiukaji:	Enye kwenda kinyume na utaratibu wa lugha unaozingatiwa.

VIFUPISHO NA ISHARA

*****	Sio sahihi
[ ]	Alama ya kufungia vipashio katika Kanuni ya Kufuta Mabano
{ }	Unukuzi wa mofimu
→	Kubadilika na kuwa
E	Kielezi
Kia.	Kiambishi
KKM	Kanuni ya Kufuta Mabano
ML	Mofolojia Leksia
Mwamb.	Mwambatano
N	Nomino
Ø	Mofu kapa
TY	Tafsiri Yangu
V	Kivumishi
Y_1	Kijenzi cha kwanza
Y_2	Kijenzi cha pili
Y_n	Vijenzi vinginevyo

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ..... **Error! Bookmark not defined.**

TABARUKU…….… iii

SHUKRANI…….....iv

IKISIRI……..….....v

ABSTRACT……. vi

UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU vii

VIFUPISHO NA ISHARA.....viii

YALIYOMO…….… ix

ORODHA YA VIELELEZO.....xiii

ORODHA YA MAJEDWALI.....xiv

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI…….......1

1.0 Usuli wa Mada.....1

1.1 Suala la Utafiti.....3

1.2 Malengo ya Utafiti.....4

1.3 Maswali ya Utafiti 5

1.4 Sababu za Kuchagua Mada 5

1.5 Upeo na Mipaka 6

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada 7

1.6.1 Maandishi ya Kijumla Kuhusu Uundaji wa Nomino Ambatani 7

1.6.2 Tafiti Kuhusu Kanuni ya Kufuta Mabano ya Mofolojia Leksia 9

1.6.3 Tafiti Bayana Kuhusu Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kufuta Mabano ..11

1.7 Misingi ya Kinadharia 13

1.7.1 Nadharia ya Mofolojia Leksia.....13

1.8 Mbinu za Utafiti 20

1.8.1 Muundo wa Utafiti 20

1.8.2 Eneo la Utafiti 20

1.8.3 Uteuzi wa Sampuli 21

1.8.4 Mbinu ya Ukusanyaji Data 21

1.8.5 Maadili ya Utafiti 22

1.8.6 Uchanganuzi wa Data 22

1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo 22

1.9 Hitimisho 23

SURA YA PILI: NOMINO AMBATANI ZINAZOKIUKA KANUNI YA KUFUTA MABANO 24

2.0 Utangulizi 24

2.1 Nomino Ambatani za Kiswahili Zinazokiuka KKM 24

2.2 Uainishaji wa Nomino Ambatani 33

2.3 Nomino Ambatani Sahili 33

2.3.1 Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Nomino 37

2.3.2 Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Kivumishi 38

2.3.2.1 Umbo la Nomino kutangulia Kivumishi 39

2.3.2.2 Nomino Ambatani za Umbo la Kivumishi kutangulia Nomino 40

2.3.3 Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Kielezi 41

2.4 Nomino Ambatani Changamani 42

2.5 Mchakato wa Uambishaji Kisarufi wa Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM 43

2.6 Hitimisho 43

SURA YA TATU: SABABU ZA KUKIUKA NA KUTOKIUKA KANUNI YA KUFUTA MABANO 46

3.0 Utangulizi 46

3.1 Sababu za Baadhi za Nomino Ambatani Kukiuka KKM 46

3.1.1 Mofu ya Pili Kuonekana na Mofu ya Kwanza 46

3.1.1.1 Upatanisho wa Kisarufi 47

3.1.1.2 Mgongano wa Kiidadi wa Nomino Ambatani za Kiswahili 48

3.1.1.3 Mvutano Unaotokea katika Nomino Ambatani za Kiswahili 51

3.1.2 Muktadha wa Matumizi ya Nomino Ambatani 53

3.2 Sababu za Nomino Ambatani Zingine Kuonekana Kutokiuka KKM 54

3.2.1 Mofu ya Pili ya Nomino Ambatani kuwa na Mofu Kapa 54

3.2.2 Nomino Ambatani Zisizopachikwa Kiambishi cha Wingi katika Mofu ya Pili 56

3.3 Hitimisho 58

SURA YA NNE: MCHANGO WA UKIUKAJI WA KANUNI YA KUFUTA MABANO 59

4.0 Utangulizi 59

4.1 Kueleza Dhima ya Shadda katika Nomino Ambatani 59

4.2 Kuonesha Uhusiano wa Fonolojia, Mofolojia, Sintaksia na Semantiki 62

4.3 Kutofautisha Utaratibu wa Uundaji wa Nomino Ambatani za Kiswahili 65

4.3.1 Utaratibu wa Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM 66

4.3.2 Utaratibu wa Nomino Ambatani Zisizokiuka KKM 67

4.4: Utaratibu wa Nomino Ambatani Zisizokiuka KKM 67

4.4 Hitimisho 69

SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI 71

5.0 Utangulizi 71

5.1 Muhtasari wa Utafiti 71

5.2 Matokeo ya Utafiti.....74

5.3 Mapendekezo.....79

5.4 Hitimisho.....80

Marejeleo…….......81

VIAMBATISHO…….....86

Kiambatisho A: Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM 86

Kiambatisho B: Nomino Ambatani Zisizokiuka KKM.....87

Kiambatisho C: Vibali ya Utafiti.....88

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1.1: Kanuni ya Kufuta Mabano 9
Kielelezo 1.2: Uundaji wa Maneno Kimsonge 14
Kielelezo 1.3: Ngazi na mizunguko katika leksia 15
Kielelezo 2.1: Utaratibu wa Uundaji Nomino Ambatani ‘Mjamzito’ 26
Kielelezo 2.2: Uwekaji Upya wa Shadda katika ‘Mkazamjomba’ 29
Kielelezo 2.3: Mabadiliko ya Mahali pa Kuweka Upya Shadda 30
Kielelezo 2.4: Uhusiano wa Kimofolojia na Kifonolojia 36

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM.....25
Jedwali 2.2: Uwekaji wa Shadda katika Nomino Ambatani.....29
Jedwali 2.3: Nomino Ambatani Sahili.....34
Jedwali 2.4: Uhusiano wa Fonolojia na Mofolojia.....35
Jedwali 2.5: Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Nomino.....37
Jedwali 2.6: Maumbo ya Nomino kutangulia Kivumishi.....39
Jedwali 2.7: Maumbo ya Kivumishi kutangulia Nomino.....40
Jedwali 2.8: Maumbo ya Nomino na Kielezi.....41
Jedwali 2.9: Nomino Ambatani Changamani.....42
Jedwali 3.1: Mofu ya Pili Kuonekana na Mofu ya Kwanza.....47
Jedwali 3.2: Nomino Ambatani za Ngeli A-WA na KI-VI.....49
Jedwali 3.3: Mofu Tofauti Zinazochukua Viambishi vya wingi.....51
Jedwali 3.4: Muktadha wa Matumizi ya Nomino Ambatani.....53
Jedwali 3.5: Mofu ya Pili kuwa na Mofu Kapa.....55
Jedwali 3.6: Mofu za Pili Zisizochukua Viambishi vya Wingi.....57
Jedwali 4.1: Uwekaji wa Shadda katika Nomino Ambatani za Kiswahili.....60
Jedwali 4.2: Uhusiano wa Fonolojia, Mofolojia, Semantiki na Sintaksia.....62
Jedwali 4.3: Utaratibu wa Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM.....66

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Mada

Mada ya utafiti huu inapatikana katika eneo jumla la mofolojia. Mofolojia ni utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa maneno (Habwe & Karanja, 2004). Haspelmath & Sims (2013) wanaeleza mofolojia kama utanzu wa isimu unaochunguza muundo wa ndani wa maneno. Kutokana na fasili hizi mtafiti anakubaliana na mawazo ya wataalam hawa kuwa mofolojia ni tawi la isimu ambalo hujihusisha na maumbo ya maneno. Mofolojia kama taaluma imegawanywa katika matawi mawili makuu: mofolojia ya minyambuliko ya maneno na mofolojia ya uundaji wa maneno. Mofolojia ya minyambuliko ya maneno hushughulika na mchakato wa minyambuliko ya maneno ambayo huwekwa kwenye mizizi ya maneno kuwakilisha maana mbalimbali lakini minyambuliko hiyo haibadili aina ya neno hilo. Mofolojia ya uundaji wa maneno ni eneo ambalo hushughulikia mikondo na matokeo ya kiisimu ya uundaji wa maneno kwa kuweka viambishi katika mizizi ya maneno, na kiambishi nyambuaji huunda neno jipya (Mgullu, 1999; Katamba & Stonham, 2019).

Uundaji wa maneno katika Kiswahili hufanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali. Mbinu hizi huwa na utaratibu maalumu wa kuzalisha maumbo yenye sifa tofauti. Mbinu hizo ni kama; utohozi, ufupishaji ambao ni wa aina tatu (akronimu, uhulutishaji na mkato), kupanua maana ya maneno, toponimu, eponimu, unyambuaji na mwambatano (Rubanza, 1996; Buberwa, 2011b; Matinde, 2012).

Mbinu ya mwambatano hutumia maneno kamili yaliyoundwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kama malighafi ya kuunda maneno mengine mapya kabisa. Maumbo

yanayozalishwa huandikwa kwa kuunganisha maneno mawili, kwa kutumia vistari au kuacha nafasi kati ya maneno yaliyoambatanishwa (Gichuru, 2010). Hata hivyo, katika utafiti huu, mtafiti aliamua kuandika nomino ambatani hizi katika namna mbili yaani; kuunganisha maneno yote na kutenganisha baadhi ya maneno katika nomino ambatani hizi ili kurahisisha uchanganuzi wa data uliofanyika. Mgullu (1999) anatazama nomino ambatani kama mofu changamano. Anaendelea kusema kuwa mofu changamano ni mofu ambazo huundwa kwa kuweka pamoja angalau mashina au mizizi miwili ya maneno ambayo katika mazingira mengine mashina hayo yanaweza kutenganishwa na kila moja likawa ni neno kamili. Maoni ya Mgullu (keshatajwa) yanaoana na yale ya Mustafa (2020) ambaye anashikilia kuwa nomino ambatani ni nomino zilizoundwa kwa kuunganisha maneno mawili (mizizi, kiini, mofimu huru au viambatisho vya leksia). Maneno mawili haya huweza kuwa na nafasi, bila nafasi au kistariungio.

Kanuni ya Kufuta Mabano ni mhimili ambao hutumiwa kuonesha hatua za kuunda neno kubalifu kwa kutumia viambajengo vyake. Mabano katika kanuni hii, huashiria mipaka ya vipashio mbalimbali na hubomolewa baada ya neno kuundwa (Katamba & Stonham, 2019). Kanuni ya Kufuta Mabano huwa na mkabala ambao unasisitiza kuwa mabano ya katikati huwa ya kwanza kufutwa katika kiwango cha leksia. Kutokana na matokeo ya mkabala huu, maneno yanayoingiliana katikati mwa ngazi leksia hayawezi kuathiriwa na sheria za fonolojia mzunguko (Kiparsky, 1982; Katamba & Stonham, 2019).

Baada ya kufuta mabano, maneno yanayotokana na mofolojia na kaida za uundaji wa maneno hayawezi kufikia muundo wa ndani wa maneno. Mkabala huu unaruhusu urejeleaji wa nje wala si ndani ya neno baada ya mabano kufutwa. Mofimu ya kwanza

katika neno zima huweza kuwekwa katika hali ya wingi bila kuingia katika mofimu ya pili katika neno zima (Allen, 1978; Siegel, 1974). Mofimu ya kwanza tunayorejelea hapa ni kiambishi cha ngeli kinachopatikana katika neno la kwanza la nomino ambatani, na mofimu ya pili ikiwa ni sehemu ya nomino ambatani inayobeba mzizi au shina la neno la kwanza pamoja na neno la pili au tatu katika neno ambatani, mathalan nomino ambatani ‘mwanamke’ ina mofimu mbili ambazo ni *{mw}* ikiwa mofu ya kwanza na *{anamke}* mofimu ya pili.

Utafiti huu ulichunguza baadhi za nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM kwa kuchukua viambishi vya mofimu za wingi katika maneno yote yanayounda nomino ambatani husika ambayo ni kinyume na Kanuni ya Kufuta Mabano inayoruhusu uchukuaji wa viambishi vya wingi katika mofimu ya kwanza pekee katika neno husika. Hii ndiyo mada ya utafiti uliochunguzwa na mtafiti.

1.1 Suala la Utafiti

Mabano katika Kanuni ya Kufuta Mabano hutumiwa kuonesha mipaka ya vipashio mbalimbali na hufutwa baada ya neno kuundwa. Kanuni hii hukubali kuwa katika Kiswahili urejeleaji katika neno huchukua kiambishi cha wingi katika kiambishi cha mofimu ya kwanza pekee ya neno husika na hairuhusu mabadiliko katikati mwa neno baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

$Y_1 \quad + \quad Y_2 \quad \rightarrow \quad [[Y_1]\,[Y_2]] \quad \rightarrow \quad [Y_1Y_2]$

Hatua 1 Hatua 2 Hatua 3

$[[mw]_{kia}.\,[ana]_{mzizi} + [[m]_{kia.}\,[ke]_{mzizi}\,]_N \rightarrow [[mwana]\,[mke]]_N \rightarrow [mwanamke]_N$

Neno ambatani kama hili lililo hapo juu linapoundwa na kufikia hatua ya 3 linakuwa na mofimu mbili tu, yaani {mw} + {anamke} kinyume ilivyokuwa katika hatua ya 1 ambapo lilikuwa na mofimu {{mw}$_{kia.}$ {ana}$_{mzizi}$ + {{m}$_{kia.}${ke}$_{mzizi}$}. Kwa mujibu wa Kanuni ya Kufuta Mabano, katika hatua ya 3 huwezi kutenga {ana} na {mke} na hivyo basi, hakuna mabadiliko yanayostahili kutokea katika mofimu hii. Katika wingi, nomino ambatani ***mw****anawake* inakuwa ***wa****na****wa****ke* ilhali tunajua kuwa katika umoja tuna mofimu mbili {mw} na {anamke}, mabadiliko haya katikati mwa mofimu {anamke} baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa huwa ni jambo la kushangaza kwani KKM hairuhusu mabadiliko kutokea katikati mwa neno baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa. Aina hii ya nomino ambatani ya Kiswahili inadhihirisha ukiukaji wa utaratibu KKM na hili ndilo suala ambalo lilichunguzwa na mtafiti. Mtafiti alinuia kuonesha kwa nini ukiukaji hutokea katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili.

1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga:

1. Kudhihirisha nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM ya Mofolojia Leksia.
2. Kudhihirisha maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM ya Mofolojia Leksia.
3. Kubainisha sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki.
4. Kueleza mchango wa ukiukaji wa KKM ya Mofolojia Leksia kwa wanaleksikografia wa Kiswahili.

1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali yaliyojibiwa na utafiti huu ni:

1. Nomino ambatani zipi za Kiswahili zinazokiuka KKM ya Mofolojia Leksia?
2. Ni maumbo yepi ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM ya Mofolojia Leksia?
3. Ni kwa sababu gani baadhi za nomino ambatani za Kiswahili hukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki?
4. Kuna mchango gani wa ukiukaji KKM ya Mofolojia Leksia kwa wanaleksikografia wa Kiswahili?

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Uundaji wa maneno ni swala muhimu katika isimu na hudhibitiwa na kanuni na utaratibu wa sarufi ya lugha husika. Mada hii iliteuliwa ili kufanikisha kueleza na kuelewa KKM ya Mofolojia Leksia katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili.

Nomino ambatani zilichaguliwa kutokana na pengo lililodhihirika na ambalo tafiti za Kiswahili hazikuwa zimetekeleza. Utafiti huu ulikuwa muhimu katika kubainisha ukiukaji wa KKM katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili.

Mada hii ni muhimu katika Kiswahili kwa sababu itawaongoza wanaleksikografia kufahamu vighairi vya Kanuni ya Kufuta Mabano ya Mofolojia Leksia ambavyo huchukua viambishi vya wingi katika mofimu zote za nomino ambatani kinyume na KKM ambayo hairuhusu urejeleaji nyuma baada ya viambajengo mbalimbali kuunganishwa.

Pia matokeo ya utafiti huu yatakuwa na umuhimu katika kupanua maarifa kuhusu utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili hasa kwa kuweka wazi jinsi fonolojia ina uwezo wa kuangalia muundo wa ndani wa maneno.

1.5 Upeo na Mipaka

Data ya uchunguzi huu ilikusanywa kutoka kwenye *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015). Kiswahili kina kamusi nyingi, zikiwemo *Kamusi ya Karne 21* (2011*)*, na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) ambazo ziliangaziwa katika utafiti wa awali. *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) ilitumiwa katika utafiti huu kwa kuwa ni kamusi mpya ambayo inasheheni misamiati ambayo kamusi zilizotangulia hazina, na kamusi hii imeshughulikia vipengele vingi ambavyo havijawahi kutumiwa na kufafanuliwa katika kamusi za awali, mathalan: kuonesha shadda na wakaa katika neno.

Maneno sitini pekee yalihusishwa katika utafiti huu ili kudhihirisha ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano na sababu za kukiuka na kuonekana kutokiuka KKM katika nomino ambatani za Kiswahili kwa kuongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya ML, yaani Kanuni ya Kufuta Mabano na Kanuni ya Mzunguko Kamili (maneno thelathini yanayokiuka KKM na thelathini yasiyokiuka KKM).

Utafiti huu ulichunguzwa kimofolojia hata ingawa matawi mengine ya isimu yaani; fonolojia, semantiki, na sintaksia yalihusishwa ili kufikia malengo ya utafiti. Fonolojia ilihusishwa na utafiti huu kutokana na madai makubwa yaliyotolewa na waitifaki wa nadharia ya Mofolojia Leksia kwamba kuna uhusiano wa upatanishi kati ya sheria ambazo zinaunda umbo la mofolojia ya neno na sheria za fonolojia zinazohusika na jinsi neno linavyotamkwa, semantiki ilihusishwa kuleta umantiki wa nomino ambatani zilizotumiwa katika utafiti huu, na sintaksia ilitusaidia kupata

uambishaji wa kisarufi katika mchakato wa kuweka nomino ambatani katika hali ya wingi.

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Usomaji mpana wa makala katika maktaba, vitabu, tasnifu na makala ya mtandao ulinuiwa kupata taarifa muhimu kuhusu ukiukaji wa KKM ya Mofolojia Leksia katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili na pia kuelewa mbinu ya mwambatano katika lugha ya Kiswahili. Maelezo yaliyopatikana yalikuwa na mashiko katika kubainisha pengo linaloshughulikiwa na utafiti huu. Sehemu hii imegawanywa katika sehemu tatu; maandishi ya kijumla kuhusu uundaji wa nomino ambatani, tafiti kuhusu Kanuni ya Kufuta Mabano ya Mofolojia Leksia na tafiti bayana kuhusu Mofolojia Leksia. Maoni ya wataalam yaliyozingatiwa ni pamoja na Gituru, (2019); Odden (2019); Katikiro (2018); Buberwa (2017); Kombe (2016); Buberwa (2011a); Gichuru (2010); Orgun & Inkelas (2002) na Kiparsky (1982).

1.6.1 Maandishi ya Kijumla Kuhusu Uundaji wa Nomino Ambatani

Akitafiti kuhusu tathmini ya maana katika maneno ambatani ya Kiswahili, Katikiro (2018) alitambua mchango wa maana za manenojenzi katika maana tokeo ya neno ambatani. Akirejelea Gordian (2010), alidai kuwa maneno ambatani hutokana na mchakato wa kimofolojia wa kuambatisha maneno mawili yaliyo tofauti kimaana na kiumbo ili kuunda neno moja jipya lenye maana moja au lenye kurejelea kitu au dhana moja. Katika utafiti huu, Katikiro (2018) alijikita katika uchunguzi wa tawi la semantiki ambapo alijikita kueleza jinsi maana katika nomino ambatani hufasiriwa. Utafiti uliotekelezwa unatofautiana na ule wa Katikiro (kehatajwa) kwa kuwa ulijihusisha na tawi la isimu la mofolojia hasa kwa kuangalia jinsi maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili hukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano. Hata hivyo, maarifa kutoka utafiti wa Katikiro (2018) yalifaa mtafiti katika kufahamu mchakato wa

kimofolojia wa uundaji nomino ambatani kwa kuambatisha maneno mawili yaliyo tofauti kimaana na kiumbo ili kuunda dhana moja.

Alikuchunguza kuhusu uambatishaji wa vishazi katika Kiswahili Kombe (2016), alibaini kuwa lugha ya Kiswahili huambatisha vipashio visivyo na hadhi sawa ikielekezwa na masharti ya mfanano kisintaksia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo ambapo alionesha jinsi maneno huambatishwa kisintaksia kuleta maana inayokusudiwa kupitia umbo la nje. Utafiti uliofanywa ni tofauti na wa Kombe (keshatajwa) kwani ulichunguza ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili. Utafiti wa Kombe (2016) ulifaa mtafiti katika kuelewa sharti la mfanano kisintaksia katika nomino ambatani za Kiswahili.

Buberwa (2011a) alitafiti kuhusu muundo wa majina ya mahali. Utafiti wake ulichunguza kifani majina ya vituo vya daladala jijini Dar es Salaam ambapo alijihusisha na mbinu za uundaji nomino kama vile; kuhamisha maana, toponimu, eponimu na mbinu ya mwambatano. Utafiti huu ulikuwa na mshabaha na utafiti uliotekelezwa kwa kuwa ulishughulikia mbinu ya mwambatano, hata hivyo, utafiti wa Buberwa (keshatajwa) ni tofauti na utafiti uliotekelezwa kwani ulichunguza nomino ambatani za Kiswahili ambazo hukiuka KKM hasa wakati nomino ambatani za Kiswahili zinapoambishwa katika hali ya wingi. Maarifa kutokana na utafiti wa Buberwa (2011a) yalisaidia mtafiti katika kuelewa dhana ya mwambatano ambayo utafiti uliotekeleza ulichunguza.

1.6.2 Tafiti Kuhusu Kanuni ya Kufuta Mabano ya Mofolojia Leksia

Orgun & Inkelas (2002) walieleza kuwepo kwa sababu za kutazama tena ufutaji mabano. Katika makala yao, walieleza kwa kufafanua kazi za awali za wataalamu Siegel (1974), Allen (1978), Pesetsky (1979), Kiparsky (1982), Mohanan (1986), Inkelas (1990) na Booij (1997). Katika utafiti wao walieleza kuhusu ufutaji wa mabano ambapo waligundua kuwa ufutaji mabano haujapewa uzingativu mwingi katika mofolojia ya maneno. Walidhihirisha kauli hii kwa kurejelea Pesetsky (1979) ambaye alieleza kuwa mkabala wa kufuta mabano unaruhusu fonolojia kurejelea mipaka iliyotolewa na ujenzi wa mofolojia wa nje, lakini hauruhusu urejeleaji wa muundo wa ndani ulioingia zaidi (TY). Utaratibu huu ulielezwa kwa mchoro ufuatao.

Kielelezo 1.1: Kanuni ya Kufuta Mabano



Asili: Orgun & Inkelas (2002:116)

Kielelezo 1.1 kinaashiria kuwa mkabala wa kufuta mabano unaruhusu fonolojia kurejelea ujenzi wa mofolojia wa nje pekee lakini hauruhusu urejeleaji wa muundo wa ndani baada ya vipashio kuunganishwa.

Utafiti wa Orgun &Inkelas (keshatajwa) ulijihusisha na kueleza namna vitenzi vya Kiingereza hukuika KKM hasa katika mchakato wa uambishaji ambapo walitambua

viambishi awali kuonekana na viambishi vya nje. Hivyo basi, utafiti wa Orgun &Inkelas (2002) ni tofauti na utafiti uliotekelezwa kwani ulijikita katika kueleza jinsi baadhi za nomino ambatani za Kiswahili hukiuka KKM, maumbo ya nomino ambatani, sababu za kukiuka na kutokiuka KKM na mchango wa ukiukaji wa KKM kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Maarifa kutokana na uchunguzi wa Orgun &Inkelas (2002) yalifaa utafiti uliotekelezwa hasa katika kueleza sababu za ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika uundaji wa nomino ambatani.

Kiparsky (1982) alieleza kuhusu mkabala wa kufuta mabano ambao unasisitiza kwamba mabano ya katikati huwa ya kwanza kufutwa katika kiwango cha leksia. Kama matokeo ya mkabala huu, maneno yanayoingiliana katikati mwa ngazi leksia hayawezi kuathiriwa na sheria za fonolojia mzunguko. Anaendelea kusema kuwa baada ya mabano kufutwa, maneno yanayotokana na mofolojia huchukuliwa kana kwamba yalibuniwa. Kwa maoni ya Kiparsky (keshatajwa), utasa huu unaenea kwa michakato ya mofolojia na kaida za kuunda maneno haiwezi kufikia muundo wa ndani wa maneno ambayo yalitokana na kiwango kilichotangulia (TY). Utafiti wa Kiparsky (1982) ulijihusisha na kueleza kwa uwazi utaratibu unaohusika katika KKM hasa maneno yanapoundwa, hali ambayo ni tofauti na utafiti uliotekelezwa kwani mtafiti alijikita katika kueleza jinsi mkabala KKM hukiukwa hasa nomino ambatani za Kiswahili zinapoambishwa katika hali ya wingi, yaani uwekaji wazi wa maumbo ya nomino ambatani kwa fonolojia. Maarifa kutokana na uchunguzi wa Kiparsky (1982) ulisaidia mtafiti katika kuelewa mchakato mzima KKM hasa wakati nomino ambatani zinapoambishwa katika hali ya wingi.

1.6.3 Tafiti Bayana Kuhusu Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kufuta Mabano

Gituru (2019) akichunguza kuhusu unyambulishaji wa vitenzi katika Kigĩchũgũ, alitambua mifanyiko na mifuatano ya vitenzi vya Kigĩchũgũ katika mchakato wa unyambuzi kwa kuongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo. Aidha, katika uchunguzi huu alidhihirisha kuwa Kanuni ya Kufuta Mabano huonesha mageuzi ya vitenzi yanayotokea katika mchakato wa unyambuzi, na maumbo mbalimbali huungana kuwa kitenzi kimoja. Utafiti wa Gituru (keshatajwa) ulijikita katika kuchambua mchakato wa unyambuaji ya vitenzi vya Kigĩchũgũ ambao ni tofauti na utafiti uliotekelezwa kwani ulihusika na kuonesha namna baadhi za nomino ambatani hukiuka KKM. Maarifa kutoka utafiti wa Gituru (2019) ulikuwa ni msingi wa kueleza utaratibu wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika mchakato wa uundaji wa maneno na maelezo zaidi kuhusu nadharia ya Mofolojia Leksia.

Odden (2019) katika uchunguzi wake kuhusu kutabiri toni katika Kikuria, alitambua Kanuni ya Kufuta Mabano hukiukwa katika uwekaji wa toni katika vitenzi vya Kikuria hasa sheria ya kuondolewa kwa shina inapokuwa wazi kwa mabano ya ndani ya shina. Anaendelea kusema kuwa hali hii hutokea wakati toni huondolewa kutoka kiambishi kuwekwa upya katika shina la kitenzi cha Kikuria na hivyo basi, hukiuka KKM ambayo hairuhusu fonolojia kurejelea mofolojia ya ndani ya neno. Utafiti wa Odden (keshatajwa) ulijihusisha na kuonesha jinsi vitenzi vya Kikuria hukuika KKM hasa katika mchakato wa uwekaji toni, hali ambayo ni tofauti na utafiti uliotekelezwa kwa kuwa mtafiti alijihusisha kuonesha jinsi nomino ambatani za Kiswahili hukiuka KKM ya Mofolojia Leksia hasa zinapoambishwa katika hali ya wingi. Maarifa kutoka utafiti wa Odden (2019), yalifaa mtafiti katika kuelewa mchakato mzima wa uundaji

wa nomino ambatani na namna baadhi za nomino hizi hukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano kwa kuweka wazi mofolojia ya ndani ya neno kwa fonolojia.

Gichuru (2010) alitekeleza utafiti unaoangazia suala la uchanganuzi wa nomino ambatani za Kiswahili. Utafiti wake ulilenga kuchanganua nomino ambatani kwa madhumuni ya kubainisha na kuainisha taratibu pamoja na kanuni zinazohusika katika uundaji wa nomino ambatani kwa kuongozwa na mihimili sita ya nadharia ya Mofolojia Leksia. Pia alidondoa data yake katika *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* (2004) na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004). Utafiti huo ulitilia mkazo maumbo ya nomino ambatani, kanuni na taratibu zilizohusika katika kuunda nomino ambatani na uhusiano wa kisarufi uliopo baina ya vijenzi vya nomino ambatani. Ni kweli kwamba utafiti wa Gichuru (2010) unakaribiana na uchunguzi uliotekelezwa kwa kuwa tafiti hizi zilitumia data ya aina moja yaani nomino ambatani na nadharia ya Mofolojia Leksia.

Hata hivyo, tafiti hizi zina tofauti kwani Gichuru (2010) alijikita katika uchanganuzi wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili na uambishaji wake kisarufi ilhali utafiti huu ulihusika na kuchunguza nomino ambatani zilizokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano kwa kuchukua viambishi vya wingi katika mofu zote zinazounda nomino husika. Hili lilichunguzwa kupitia malengo yafuatayo; kudhihirisha nomino ambatani zinazokiuka KKM ya ML, kudhihirisha maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM ya Mofolojia Leksia, kubainisha sababu za baadhi za nomino ambatani hukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki na mchango wa ukiukaji KKM ya Mofolojia Leksia kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Maarifa kuhusu nomino ambatani na nadharia ya Mofolojia Leksia kutoka kwa utafiti wa Gichuru (2010) yalikuwa ya kufaa katika utafiti wa mada hii teule.

1.7 Misingi ya Kinadharia

Njia mwafaka ilizingatiwa wakati wa uteuzi wa nadharia bora itakayoongoza mchakato mzima wa utafiti huu. Mtafiti aliteua nadharia yenye uwezo wa kueleza vigezo huria na vigezo geu ambavyo huamabatana na malengo ya utafiti. Nadharia iliyohitajika ni ile iliyokuwa na uwezo wa kudhihirisha baadhi za nomino ambatani zinazokiuka KKM, maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM, sababu za kukiuka na kutokiuka KKM na mchango wa ukiukaji wa KKM kwa wanaleksikografia wa Kiswahili.

1.7.1 Nadharia ya Mofolojia Leksia

Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksia iliyoanzishwa na Kiparsky (1982) na kufafanuliwa zaidi na Katamba & Stonham (2019). Nadharia ya ML ilianzishwa ili kufidia mtazamo wa Chomsky wa Sarufi Zalishi ambao haukutambua tawi la mofolojia kama tawi mahususi la lugha. Kimsingi nadharia hii inaonyesha uhusiano wa kaida zinazounda maumbo ya kimofolojia na kaida zinazotawala jinsi maumbo hayo yanavyotamkwa (Kiparsky, 1982; Katamba & Stonham, 2019). Kaida katika leksia zimepangwa kwenye ngazi kimsonge (Kiparsky, 1982; Katamba & Stonham, 2019; Mcmahon, 2000). Hali hii huashiria kwamba viambishi (mofimu) vinavyopachikwa katika mzizi ili kuunda neno hupangwa kidaraja.

Nadharia hii imetambua viwango viwili vya kanuni; kanuni leksika ambazo hujihusisha na kuunda neno kubalifu kileksika na kanuni kirai kwa upande mwingine huhusika na utendaji kazi baada ya neno kuundwa. Mihimili ya nadharia hii ni sita. Utafiti huu uliongozwa na mihimili miwili: mhimili wa Kanuni ya Kufuta Mabano na

mhimili wa Kanuni ya Mzunguko Kamili. Hata hivyo, mtafiti alitatoa maelezo ya mihimili minne ili kupata umaizi wa nadharia ya Mofolojia Leksia.

(i) Kanuni ya Ngazi Leksia

Kulingana na Kiparsky (1982), Katamba (1989), Katamba & Stonham (2019) na Mcmahon (2000), kanuni ya ngazi leksia huchukulia kuwa vipashio vya kuunda maneno vimepangwa katika ngazi kimsonge na vipashio hivi huunganishwa hatua kwa hatua na kujenga vipashio vikubwa zaidi kama ifuatavyo katika Kielelezo cha 1.2.

Kielelezo 1.2: Uundaji wa Maneno Kimsonge



Kielelezo 1.2 kinadhihirisha ngazi tatu ambapo ngazi ya kwanza hushughulikia unyambuzi na uambatizi unaoongozwa na sheria ghairi. Ngazi ya pili hushughulika na unyambuzi unaozingatia kanuni dhahiri na uambatani, na ngazi ya tatu inashughulika na uambatizi wa kisarufi unaozingatia sheria dhahiri (Kiparsky, 1982). Kila ngazi katika kielelezo hiki huwa na vipashio vyenye sifa maalumu kulingana na athari za kifonolojia. Mhimili huu haukutumika katika utafiti uliotekelezwa.

(ii) Kanuni ya Mzunguko Kamili

Mhimili wa Kanuni ya Mzunguko Kamili husisitiza ukuruba wa sheria za mofolojia na fonolojia katika kila ngazi ya leksia. Kielelezo 1.3 kinaonesha ngazi na mizunguko katika leksia kama ifuatavyo:

Kielelezo 1.3: Ngazi na mizunguko katika leksia



Asili: (Kiparsky, 1982:133)

Katika kanuni hii, kaida hutawala kila ngazi mpaka neno kubalifu kuundwa kabla ya kupitishwa kwa ngazi inayofuata. Kaida hizi hutawala mchakato wa ngazi hiyo na huwa hazina ufikiaji na uathiriaji wa michakato katika ngazi zilizotangulia. Kila ngazi hujitosheleza kikaida na mwisho wake tunapata uundaji wa neno kubalifu (Kiparsky,

1982). Mwambatano hutokea katika ngazi ya pili pamoja na mkazo kupachikwa katika nomino ambatani husika baada ya viambajengo vya neno husika kupitia ngazi ya kwanza na pili. Mhimili huu ulitumika katika utafiti huu kuonesha uhusiano wa sheria za kimofolojia na kifonolojia katika kila daraja.

(iii) Kanuni ya Ufinyu wa Sifa

Hii ni aina ya kanuni ambayo hutawala matumizi ya uwakilishaji wa sifa katika maumbo. Katika kanuni hii, cha msingi ni kutowakilisha sifa zinazoweza kutabiriwa na sifa zinazopewa uzingativu zaidi ni zile zisizoweza kutabirika. Kwa mfano, katika kuunda neno ‘mpasi’ kutoka kwa {mu + pat + i}, neno *mupati linaundwa kwanza na baada ya neno hilo kupitia mabadiliko ya kifonolojia sauti /i/ huvuta mbele sauti /t/ na kuifanya itamkiwe katika kaakaa gumu kama ifuatavyo:

/t/ → /s/ — /i/

t s i

$$\begin{bmatrix} + \text{kizuiwa} \\ + \text{ufizini} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} + \text{kikwamizwa} \\ + \text{kaakaa gumu} \end{bmatrix} \diagup\!\!\!

(iv) Kanuni ya Kwingineko

Katamba & Stonham (2019) wanaeleza kuwa kanuni ya kwingineko hujihusisha na utumikizi wa sheria mbalimbali katika ngazi fulani na kila ngazi huwa zinadhibitiwa na kaida maalumu. Katika hali ambapo sheria mbili zinang'ang'ania nafasi ya kiutendakazi, sheria iliyo ya kimsingi zaidi hutangulia iliyo ya kijumla ambayo hutenda kazi kwingineko. Kwa mfano, katika uambishaji unaotokea katika ngazi za kwanza, kanuni za kimsingi zinapewa uzingativu na kuzuia kutumikiza kanuni za kijumla ambazo zinatumika kwingineko, yaani ngazi ya pili. Kanuni hii inazuia kuundwa kwa maneno kama *mpati.

[Kiambishi {m} + {pat-} kinominishi {i}]→ mpasi (*mpati).

Pia mhimili huu haukutumiwa katika utafiti huu.

(v) Kanuni ya Kuhifadhi Muundo

Hii ni kanuni ambayo husisitiza kuwa baada ya utumikizi wa sheria za fonolojia na mofolojia katika uundaji wa maneno, sharti muundo wa lugha husika uhifadhiwe yaani neno linaloundwa katika kila daraja liafiki muundo wa sarufi ya lugha husika, mathalani, Kiswahili. Kutokana na sharti la muundo kuhifadhiwa, kanuni hii hudhibiti uundaji wa neno au maneno lisiloafiki mpangilio wa lugha husika. Mathalan, kanuni hii huzuia uundaji wa neno kama vile ***mwmkeenza** katika sarufi ya Kiswahili kwa kuwa halikubaliki katika mpangilio wa sarufi ya lugha husika. Mhimili huu haukutumika katika utafiti huu.

(vi) Kanuni ya Kufuta Mabano

Mhimili huu ndio suala la utafiti lililochunguzwa. Kanuni hii huonyesha hatua zinazotumiwa katika kuunda neno sahihi kwa kutumia vipashio vyake. Mabano

hutumiwa kuonesha mipaka ya vipashio mbalimbali na mabano hubomolewa baada ya neno kuundwa (Katamba & Stonham, 2019). Kanuni hii ni muhimu katika uundaji wa maneno kwani huonesha jinsi mashina mbalimbali yanavyoambatishwa na kuunda neno kamili kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

$[Enye]_V$ $[kiti]_N$ Hatua 1

↓

$[[Mw]$ $[enye]]_V$ $[kiti]_N]_N$ Hatua 2

↓

$[Mwenyekiti]_N$ Hatua 3

↓

Mwenyekiti Hatua 4

Kinachodhihirika hapa juu ni kuwa vipashio mbalimbali huunganishwa kuanzia hatua ya kwanza mpaka hatua ya tatu ambapo mabano hubomolewa na hatua ya nne ndio hatua ya mwisho ambapo tunapata neno kamili ‘mwanamke.’

Pesetsky (1979) anadai kuwa katika Kanuni ya Kufuta Mabano; mkabala wa kufuta mabano unaruhusu fonolojia kurejelea mipaka iliyotolewa na ujenzi wa mofolojia wa nje, lakini hairuhusu kurejelea muundo wa ndani wa neno zima. Kwa hali hii, ufutaji mabano huweka mipaka kati ya vijenzi vinavyotokea kuonekana, wakati huo kutoruhusu urejeleaji kabisa wa vijenzi vya ndani ya muundo wa neno jipya.

Kiparsky (1982) anaeleza kuhusu mkabala wa Kanuni ya Kufuta Mabano ambapo anasisitiza kuwa mabano ya ndani yafutwapo mwisho wa kiwango cha leksia,

hayawezi kuathiriwa na sheria za fonolojia ya mzunguko. Baada ya kufuta mabano, maneno yanayotokana na mofolojia huchukuliwa kana kwamba yalibuniwa. Kwa maoni ya Kiparsky (1982), utasa huu unaenea kwa michakato ya mofolojia na kaida za kuunda maneno haziwezi kufikia muundo wa ndani wa maneno yaliyotokana na kiwango kilichotangulia.

Katika uchunguzi uliotekelezwa mtafiti alibainisha baadhi za nomino ambatani zinazokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano hasa zinapochukua mofimu za wingi kwa maneno yote yanayounda neno husika kama utaratibu ufuatao unavyoonesha:

$$[\text{wingi} + Y_1] + [\text{wingi} + Y_n]$$

Maelezo: Kijenzi tangulizi (neno kuu) pamoja na vijenzi vingine (Y_n) vinaongezwa viambishi vya kiidadi katika upande wa kushoto wa kila kijenzi (Gichuru, 2010).

Kinachodhihirika wazi kutokana na maelezo ya hapo juu ni kuwa maneno yote yanayounda nomino husika yanabadilika katika wingi kinyume na Kanuni ya Kufuta Mabano ya Mofolojia Leksia ambayo hushikilia kuwa baada ya mabano kufutwa sheria za kimofolojia haziwezi kurejelea hali za ndani za muundo wa kimofolojia wa awali. Ufuatao ni mfano wa nomino ambatani inayokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano:

Umoja	**Wingi**
[**Mw** [enye**ki**ti]]	[**W** [enye**vi**ti]]

Hapa kinachodhihirika ni kuwa uambishaji kisarufi una uwezo wa kuangalia nyuma, kinyume na Kanuni ya Kufuta Mabano inayoshikilia kuwa uambishaji wa kisarufi hauna uwezo wa kuangalia nyuma na iwapo utaangalia nyuma huchukua mofimu za wingi katika mofimu ya kwanza pekee na hairuhusu urejeleaji nyuma baada ya

viambajengo mbalimbali kuunganishwa. Utafiti huu ulitumia mhimili wa Kanuni ya Kufuta Mabano na mhimili wa Kanuni ya Mzunguko Kamili katika kujibu maswali ya uchunguzi.

1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inajihusisha na kueleza mbinu zilizotumiwa katika uchunguzi huu, ili kuafikia malengo ya utafiti huu. Hasa inaeleza muundo wa utafiti, uteuzi wa sampuli, eneo la utafiti, ukusanyaji wa data, maadili ya utafiti, uchanganuzi wa data, na uwasilishaji wa ripoti ya utafiti.

1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Muundo huu ulitumiwa kudhihirisha nomino ambatani zinazokiuka KKM, kudhihirisha maumbo ya nomino ambatani yanayokiuka KKM, sababu za kukiuka na kutokiuka KKM, na mchango wa ukiukaji wa KKM kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Pia michoro na majedwali yalitumiwa kuweka wazi utaratibu wa KKM katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili na jinsi baadhi za nomino ambatani hizo hukiuka utaratibu wa KKM.

1.8.2 Eneo la Utafiti

Uchunguzi huu ulifanyika maktabani. Mtafiti alitembelea maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta ili kusoma kazi zilizoandikwa kuhusu mada ya utafiti huu. Maktabani mtafiti alisoma; tasnifu, majarida, vitabu, na makala mbalimbali ili kupata hoja za kutosha za kueleza Kanuni ya Kufuta Mabano na mchakato mzima wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili. Pia mtandao ulisakurwa kwa madhumuni kwamba makala za hivi karibuni zinazolenga mada ya utafiti zilisomwa, na hili liliafikiwa kwa kuwa maswali ya utafiti yalijibiwa ipasavyo.

1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Mugenda na Mugenda (2019) wanaeleza kuwa sampuli ni kitu kimoja kinachochaguliwa katika vitu vingi kwa ajili ya kuwakilisha jamii au kundi zima. Creswell (2007) anaeleza sampuli ya kimakusudi kama aina ya sampuli iliyoteuliwa na mtafiti kwa misingi ya sifa anazozitafitia katika jumuia yake. Mtafiti anakubaliana na maoni haya ya Creswell (2007) kuhusu fasili ya sampuli ya kimakusudi na mawazo yake yalifaa katika utafiti huu. Mtafiti alitumia sampuli ya kimakusudi kuteua nomino ambatani za Kiswahili kutoka *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015), yaani maneno sitini; thelathini nomino ambatani zinazokiuka KKM na thelathini zisizokiuka KKM yalisampulishwa ili kupata data yenye sifa sawia.

Sababu ya kuteua maneno sitini pekee katika utafiti uliotekelezwa ni kutokana na kuongozwa na maoni ya Kothari (2004) ambaye anasema kuwa asilimia 10% kutoka jumuiya hutumiwa kama sampuli teule ya utafiti unaokusudiwa kufanywa. Kutokana na utafiti wa awali, nomino ambatani 30 pekee katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) hukiuka KKM. Hivyo basi, mtafiti alitumia nomino ambatani zote 30 ilhali katika nomino ambatani zisizokiuka KKM asilimia 10% ilitumika kwa kuwa nomino ambatani jumuiya ni 300 na hivyo maneno 30 yalitumika. Pia Milroy (1987) anapendekeza sampuli ndogo kutumiwa katika uchunguzi ili kujiepusha na urudiaji mwingi na uchunguzi haufai kuwa na data chache. Kutokana na maoni ya Milroy (1987) ni wazi kuwa data wastani ilifaa katika utafiti huu.

1.8.4 Mbinu ya Ukusanyaji Data

Mtafiti alitumia mbinu ya upekuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji wa data yake ambapo alidondoa nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM na zile ambazo hazikiuki KKM ya ML kutoka *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) kwa usaidizi wa vifaa

vya kuhifadhi maandiko yaani kalamu na kitabu. Mtafiti aliteua nomino ambatani sitini yaani thelathini zinazokiuka KKM na thelathini zisizokiuka KKM kwa msingi wa maumbo yake hasa jinsi zinapochukua viambishi vya wingi wakti zinapoambishwa katika hali ya wingi.

1.8.5 Maadili ya Utafiti

Utafiti huu ulizingatia maadili kwa kuhakikisha kuwa kazi zote zilizorejelewa katika utafiti uliotekelezwa zilijumuishwa katika marejeleo. Kuhakikisha kuwa utafiti uliotekelezwa haujawasilishwa katika chuo chochote, mtafiti alisakura mada ya utafiti huu mtandaoni na kubaini haujafanywa. Mwisho, matokeo katika utafiti huu yatakuwa yenye uyakinifu bila kuwa na mapendeleo yoyote. Pia mtafiti aliomba kibali cha utafiti kutoka afisi husika za utawala ili kufanikisha uchunguzi huu.

1.8.6 Uchanganuzi wa Data

Data katika hatua hii iliwekwa katika makundi mbalimbali ambapo kwanza mtafiti alibainisha nomino ambatani zinazokiuka KKM na nomino ambatani zisizokiuka KKM hasa zile zinazochukua viambishi vya wingi katika mofimu za kwanza za maneno husika. Baada ya kukusanya data, ilichanganuliwa katika misingi ya KKM na Kanuni ya Mzunguko Kamili ya nadharia ya Mofolojia Leksia. KKM na Mzunguko Kamili ilitumikizwa kuonesha utaratibu unaohusika katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili na sheria zinazotawala mchakato mzima wa uundaji wa nomino ambatani. Ili kufikia malengo ya utafiti uliotekelezwa, uchanganuzi ulilenga kujibu maswali yaliyoongoza utafiti huu.

1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya uchunguzi huu yalitolewa kwa njia ya maelezo, majwedali na michoro, ambapo michoro na majedwali yalitumiwa kutoa taarifa zaidi kuhusu maelezo

ndiposa malengo ya utafiti yakaafikiwa na hili lilidhihirisha ufaafu wa utafiti uliotekelezwa katika taaluma ya isimu. Njia za uwasilishaji wa matokeo zilitilia maanani malengo ya utafiti ambayo ni: kudhihirisha nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM ya Mofolojia Leksia, kudhihirisha maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM, kubainisha sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki, na kueleza mchango wa ukiukaji wa KKM ya Mofolojia Leksia kwa wanaleksikografia wa Kiswahili.

1.9 Hitimisho

Sura hii imetalii utaratibu uliofuatwa kuhakikisha maswali ya uchunguzi huu yamejibiwa. Sura hii imeeleza usuli wa mada, suala la utafiti, madhumuni ya uchunguzi, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, mapitio ya maandishi, misingi ya kinadharia, na mbinu za uchunguzi zilizotumiwa. Sura ya Pili ifuatayo imeshughulika na kudhihirisha nomino ambatani zinazokiuka KKM na maumbo ya nomino ambatani husika.

SURA YA PILI

NOMINO AMBATANI ZINAZOKIUKA KANUNI YA KUFUTA MABANO

2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia nomino ambatani za Kiswahili ambazo zinakiuka KKM kwa kuruhusu mabadiliko kutokea katikati mwa neno baada ya viambajengo mbalimbali kuunganishwa. Mabadiliko haya hutokea pale ambapo mofimu ya pili katika nomino ambatani huchukua viambishi vya wingi, hali ambayo ni kinyume na Kanuni ya Kufuta Mabano inayoruhusu fonolojia kurejelea mipaka ya nje kabisa iliyowekwa katika uundaji wa kimofolojia wa neno, na hushikilia kuwa baada ya mabano ya katikati kufutwa kaida za kuunda maneno haziwezi kufikia muundo wa ndani wa maneno. Lengo kuu katika sura hii, ni kudhihirisha nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM na maumbo ya nomino hizi kwa kuongozwa na mihimili miwili; Kanuni ya Kufuta Mabano na Kanuni ya Mzunguko Kamili ya Mofolojia Leksia (Pesetsky, 1979; Kiparsky, 1982).

2.1 Nomino Ambatani za Kiswahili Zinazokiuka KKM

Katika utafiti uliotekelezwa maktabani, mtafiti alibaini nomino ambatani thelathini ambazo zinakiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ambazo zimeorodheshwa katika Jedwali 2.1.

Jedwali 2.1: Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM

Nomino ambatani (Umoja)	**Nomino Ambatani (Wingi)**
[**Mw** [ana**m**ke]]	[**wa** [ana**wa**ke]]
[**M** [ja**m**zito]]	[**wa** [ja**wa**zito]]
[**Ø [**raia **mw**ema]]	[**ø** [raia **w**ema]]
[**Mw** [alimu **m**kuu]]	[**w** [alimu **wa**kuu]]
[**Mw** [enye**ki**ti]]	[**w** [enye**vi**ti]]
[**M** [ke**mw**enza]]	[**wa**] [ke**we**nza]]
[**Mw** [ana**m**kaidi]]	[**w** [ana**wa**kaidi]]
[**M** [kaza**mw**ana]]	[**w** [akaza**wa**na]]
[**Mw** [ana**m**falme]]	[**w** [ana**wa**falme]]
[**Mw** [ana**m**potevu]]	[**w** [ana**wa**potevu]]
[**Ki** [rai **k**ielezi]]	[**vi** [rai **v**ielezi]]
[**Ki** [rai **k**itenzi]]	[**vi** [rai **v**itenzi]
[**Ki** [rai **k**iunganishi]]	[**vi** [rai **v**iunganishi]]
[**Ki** [rai**k**ivumishi]]	[**vi** [rai **vi**vumishi]]
[**M** [kaza**m**jomba]]	[**wa** [kaza**w**ajomba]]
[**Ki** [unga**mw**ana]]	[**vi** [unga**w**ana]]
[**M** [kuu **mw**enzio]]	[**wa** [kuu **we**nzio]]
[**Mw** [ana**m**kendege]]	[**wa** [ana**w**akendege]]
[**Mw** [ana**mw**ali]]	[**w** [ana**wa**li]]
[**Mw** [anawa**mw**ana]]	[**w [**anawa**wa**na]]
[**Ø** [baba **m**dogo]]	[**ø** [baba **wa**dogo]]
[**Ø** [baba **m**kubwa]]	[**ø** [baba **wa**kubwa]]
[**Ø** [bwana **m**dogo]]	[**ø** [bwana **wa**dogo]]
[**Ø** [neno**k**uu]]	[**ma** [neno**ma**kuu]]
[**M** [hariri **m**kuu]]	[**wa** [hariri **wa**kuu]]
[**Ki** [takasa **m**kono]]	[**vi** [takasa **mi**kono]]
[**M** [sikilizaji mtazamaji]]	[**wa** [sikilizaji **wa**tazamaji]]
[**M** [saidizi mshauri]]	[**wa** [saidizi **wa**shauri]]
[**M** [tunga**m**ziki]]	[**wa** [tunga**mi**ziki]]
[**Ø** [utiwa**m**gongo]	[**ø** [utiwa**mi**gongo]]

Data ya nomino ambatani katika Jedwali 2.1 zinadhihirisha ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano. Kanuni hii, huwa na mkabala ambao unasisitiza kuwa mabano ya katikati huwa ya kwanza kufutwa katika kiwango cha leksia na iwapo urejeleaji utakuwa katika nomino ambatani, urejeleaji huu huwa katika mofimu ya kwanza pekee (Allen, 1978; Kiparsky, 1982; Katamba & Stonham, 2019). Kutoa mwanga zaidi kuhusiana na ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano, mtafiti ataeleza utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani ‘mjamzito’ kutoka Jedwali 2.1 kama kiwakilishi cha

nomino zingine ambatani ishirini na tisa zilizoorodheshwa hapa juu kama ifuatavyo katika Kielelezo 2.1:

Kielelezo 2.1: Utaratibu wa Uundaji Nomino Ambatani ‘Mjamzito’

$[[[m]_{kia}[ja]_{shina}]\ [[m]_{kia.}[zito]_{shina}]]$ Hatua 1

$[[mja]_{N}[mzito]]_{V}$ Hatua 2

$[mjamzito]_{N}$ Hatua 3

Mjamzito → *wajamzito (sio sahihi)

Wajawazito (sahihi)

Kinachodhihirika katika utaratibu huu ni kuwa hatua ya kwanza inajihusisha na kutenganisha vipashio mbalimbali kwa kutumia mabano. Mathalan, katika hatua hii viambishi katika nomino ambatani ‘mjamzito’ vimetenganishwa na shina $[[[m]_{kia}[ja]_{shina}]$ na $[[m]_{kia.}[zito]_{shina}]]$. Katika hatua ya pili, mabano ya katikati hufutwa kuonesha viambajengo vya nomino ambatani; $[[mja]_{N}[mzito]]_{V}$, na katika hatua ya tatu nomino ambatani huwa tayari imeunganishwa; $[mjamzito]_{N}$, na mabano hubomolewa kuonesha mwisho wa utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani. Baada ya kuondoa mabano, maneno yaliyoundwa kwa kuunganisha vijisehemu kimofolojia huchukuliwa kama ambayo hayajaunganishwa, yamekuwa mazima hivyo tangu awali.

Kwa mujibu wa Orgun & Inkelas (2002), mabano yafutwapo katika mchakato wa uundaji wa nomino ambatani hii, Kanuni ya Kufuta Mabano hairuhusu fonolojia kurejelea maumbo yaliyokuwa ndani, mathalan, *{jamzito}* mofimu ya pili. Kulingana na Kanuni ya Kufuta Mabano, uambishaji kisarufi wa nomino ambatani katika hali ya wingi unafaa kuwa **wajamzito*, nomino ambayo huleta utata wa maana kisarufi.

Kutoa utata huu wa maana kisarufi, nomino hii huruhusu uambishaji wa kisarufi katika mofimu ya pili yaani, {jawazito}, hali ambayo husababisha mabadiliko kutokea katikati mwa nomino ambatani *mjamzito* baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa na kuwa *wajawazito*. Hali hii hutokea katika nomino ambatani zote katika Jedwali 2.1, yaani nomino hizi huchukua viambishi vya wingi katika mofimu ya pili ya nomino ambatani.

Orgun & Inkelas (2002) wanadai kuzuka kwa nadharia inayoweka wazi mofolojia ya ndani kwa fonolojia hata baada ya neno kuundwa kikamilifu yaani nadharia ya Umbo Upeo (Prince & Smolensky, 1993). Nadharia hii hushikilia kuwa habari zote za mofolojia huonekana na fonolojia. Maoni haya yanaoana na ya Cole (1995) ambaye anasema kuwa muundo wa ndani wa mofolojia ya neno lazima uonekane ili kupata athari za mzunguko kwa kuweka vizuizi katika vikoa vilivyoainishwa kimofolojia. Maoni ya Orgun & Inkelas (2002) na Cole (1995) yanatofautiana na wataalam Siegel (1974), Allen (1978), Pesetsky (1979), Kiparsky (1982), Mohanan (1986), Inkelas (1990), Booij (1997) na Katamba & Stonham (2019) ambao wanashikilia kuwa baada ya mabano kufutwa katika mchakato wa uundaji wa neno, Kanuni ya Kufuta Mabano huruhusu fonolojia kurejelea mipaka ya nje kabisa iliyowekwa katika uundaji wa kimofolojia lakini hairuhusu kurejelea maumbo yaliyokuwa ndani. Katika utafiti huu, mtafiti alitambua uwepo wa nomino ambatani za Kiswahili ambazo hukiuka KKM kwa kuruhusu mabadiliko kutokea katika mofimu ya pili ya nomino ambatani kama zilivyoorodheshwa katika Jedwali 2.1 ambapo zinachukua viambishi vya wingi, mathalan: *mkemwenza* kuwa *wakewenza*.

Orgun & Inkelas (keshatajwa) wanaeleza namna ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano unavyodhihirika katika lugha ya Kijapani ambapo fonolojia inaonekana kuhitaji ufikiaji zaidi wa muundo wa ndani wa neno kuliko vibali vya Kanuni ya

Kufuta Mabano vinavyoruhusu fonolojia kurejelea mipaka ya nje iliyowekwa katika uundaji wa kimofolojia. Maoni ya Orgun & Inkelas (2002) yanaoana na Poser (1990) ambaye anadai kuwa shadda katika nomino za Kijapani zinazoundwa kutoka kwa vitenzi huonesha mfano wa kukomesha Kanuni ya Kufuta Mabano na sheria ya fonolojia inayotumiwa kwa unominishaji wa umbotokeo inahitaji kujua unominishaji wa pembejeo ulikuwa ambatani. Poser (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa sheria inayoweka shadda katika nomino zinazoundwa kutoka vitenzi lazima itaje mpaka wa uambatani katika mazingira yake. Wanachomaanisha Orgun & Inkelas (2002) na Poser (1990) ni hali ya kupotea kwa shadda katika nomino za Kijapani zinazoundwa kutoka kwa vitenzi. Maarifa kutokana na ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika nomino za Kijapani zilizoundwa kutoka kwa vitenzi yalifaa mtafiti kuelewa mchakato mzima wa fonolojia kurejelea maumbo ya ndani ya neno na namna nomino ambatani hizi hukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano. Jedwali 2.2 lifuatalo linadhihirisha namna shadda huwekwa katika nomino ambatani za Kiswahili.

Jedwali 2.2: Uwekaji wa Shadda katika Nomino Ambatani

Uwekaji wa Shadda kila Neno	**Uwekaji Upya wa Shadda**
'Mja + m'zito → *'mjam'zito	mjam'zito
'Mwana + 'mke → *'mwana'mke	mwana'mke
'Mwana + m'falme → 'mwanam'falme	mwanam'falme
M'kaza + m'jomba → *m'kazam'jomba	mkazam'jomba
Msikili'zaji + mtaza'maji → *msikili'zaji mtaza'maji	msikilizaji mtaza'maji
M'tunga + m'ziki → *m'tungam'ziki	mtungam'ziki
Msai'dizi +msha'uri → *msai'dizi msha'uri	msaidizi msha'uri
M'kaza + 'mwana → *m'kaza'mwana	mkaza'mwana
'Mwana + 'mke + 'ndege → *'mwana'mke'ndege	mwanamke'ndege

Kinachotokea katika Jedwali 2.2 ni kuwa kila neno huwa na shadda ya msingi kabla kuunganishwa kuwa ambatani. Katika mchakato wa uwekaji upya wa shadda katika nomino ambatani, shadda huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho katika nomino ambatani ambayo kimsingi inapatikana katika neno la pili la hapo mwanzoni kabla maneno hayo yaungane. Tutatumia ‘mkazamjomba’ kama kiwakilishi cha nomino ambatani za Jedwali 2.2 kueleza namna uwekaji upya wa shadda hutokea katika nomino ambatani. Kielelezo 2.2 kifuatacho kinadhihirisha jinsi shadda huwekwa katika utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani ‘mkazamjomba.’

Kielelezo 2.2: Uwekaji Upya wa Shadda katika ‘Mkazamjomba’

1. Maneno mawili: mkaza + mjomba
2. Shadda katika kila neno: m'kaza + m'jomba
3. Mwambatano: m'kazam'jomba
4. Uwekaji shadda upya: mkazam'jomba

Kielelezo 2.2 kinadhihirisha utaratibu wa uwekaji upya shadda katika nomino ambatani ‘mkazamjomba’ ambapo katika hatua ya kwanza nomino ambatani hizi bado hazijapachikwa shadda. Katika hatua ya pili kila neno hupachikwa shadda katika mazingira yake na zinapoambatishwa katika hatua ya tatu kila neno huwa na shadda. Hatua ya nne inadhihirisha uwekaji upya wa shadda ambapo shadda msingi huondolewa katika neno la kwanza na kupachikwa upya katika silabi ya pili kutoka mwisho ya nomino ‘mkazamjomba’ kama ilivyojitokeza katika Kielelezo 2.2.

Kutoa mwanga zaidi kuhusu mabadiliko ya uwekaji upya wa shadda, mtafiti alitumia mchoro wa mzunguko wa Mofolojia Leksia kueleza hatua za uwekaji shadda na namna shadda hupachikwa upya katika nomino ambatani za Kiswahili. Kielelezo 2.3 kifuatacho kinaonesha mabadiliko ya uwekaji upya wa shadda katika nomino ambatani ‘mkazamjomba.’

Kielelezo 2.3: Mabadiliko ya Mahali pa Kuweka Upya Shadda

	Mofolojia	Fonolojia	Mofolojia	Fonolojia
Shina		m'kaza		m'jomba
		↓		↓
Ngazi 1	[[mkaza]]	↔ [[m'kaza]]	[[mjomba]]	↔ [[m'jomba]]
		↓		↓
Ngazi 2		[[m'kaza]]		[[m'jomba]]
(Mwambatano)		[[m'kaza] [m'jomba]] ⟶ mkazam'jomba		

Kinachotokea katika Kielelezo 2.3 ni kuwa, nomino ambatani ‘mkazamjomba,’ katika mzunguko wa kwanza shadda hupachikwa katika nomino ‘mkaza’ na ‘mjomba’ yaani, [[m'kaza]] [[m'jomba]]. Katika mzunguko wa pili mabano ya ndani hufutwa; kwa mujibu wa kanuni ya mzunguko wa mabadiliko, uondoaji wa shadda ya

msingi kutoka nomino ‘mkaza’ na upachikaji upya wa shadda katika nomino ‘mjomba’ huifanya shadda msingi kuwa hafifu, na hivyo basi, shadda ya msingi huondolewa na kuwekwa upya katika silabi ya pili kutoka mwisho wa nomino ‘mjomba’ kuwa ‘mkazam'jomba.’ Chomsky & Halle (1968) wanadai kuwa wakati shadda msingi imewekwa katika nafasi fulani ya neno, basi shadda zingine katika neno hilo huwa hafifu kama inavyojitokeza katika nomino ambatani ‘mkazamjomba.’ Uondoaji wa shadda kutoka neno la kwanza na upachikaji upya wa shadda katika neno la pili katika mchakato wa Fonolojia ya Kimzunguko unadhihirisha kuwa hakuna ukiukaji wa KKM kwa sababu sheria huona hili kama neno moja, si mawili kama awali. Uondoaji wa shadda msingi katika neno la awali hautokei katika nomino ambatani za Kiswahili pekee bali katika lugha zingine kama Kihispania.

Halle, Harris na Vergnaud (1991) wanaeleza jinsi shadda huwekwa katika nomino ambatani za Kihispania kwa kuongozwa na mkabala wa kufuta shadda hasa nomino ambatani zinapoondoa shadda msingi kutoka mkono wa kulia wa kiambajengo cha nomino ambatani na kuwekwa upya katika mkono wa kushoto wa kiambajengo cha nomino ambatani husika. Mathalan kama inavyojitokeza katika nomino ambatani ya Kihispania '*agwani*'*eve* ‘theluji’ ambapo shadda ya msingi huondolewa kutoka shina '*agwa* na kuwekwa upya katika nomino *ni*'*eve* kuwa *agwani*'*eve*. Hali hii ya uondoaji wa shadda msingi kutoka neno la kwanza inadhihirika katika nomino ambatani zilizoorodheshwa katika Jedwali 2.2. Odden (2019) anadai kuwa Kanuni ya Kufuta Mabano hukiukwa katika uwekaji wa toni katika vitenzi vya Kikuria hasa sheria ya kuondolewa kwa shina inapokuwa wazi kwa mabano ya ndani ya shina kama inavyojitokeza katika vitenzi *tuùre* na *gi – tùùre* kuashiria ‘nimechukua hicho.’ Hali hii hutokea wakati toni huondolewa kutoka kiambishi na kuwekwa upya katika shina

la kitenzi cha Kikuria na hivyo basi, hukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ambayo hairuhusu fonolojia kurejelea mofolojia ya ndani ya neno.

Massamba (2011) anauita mkazo msingi ambapo unaondolewa kutoka neno la kwanza na kupachikwa upya katika neno la pili. Anaendelea kusema kuwa neno la kwanza kwa kiasi fulani katika nomino ambatani huwa limebakia na mkazo, lakini mkazo ule hauwi mkazo msingi; mkazo huo unaweza kuwa wa pili au tatu kutegemea maneno yanayounda nomino ambatani husika.

Orgun na Inkelas (2002) wanaeleza pia kuwepo kwa changamoto za matumizi ya Kanuni ya Kufuta Mabano katika uambishaji wa vitenzi vya Kiingereza ambapo walibaini baadhi ya vitenzi kuwa na viambishi awali vinavyoonekana na viambishi vya nje. Orgun na Inkelas (2002) wanaendelea kusema kuwa kiambishi cha mofimu huwa wazi kwa uwepo wa kiini cha mofimu nyingine maalumu, yaani aina hizi za vitenzi huhitaji umbo la ndani la shina kuonekana na mofimu ya nje.

Hali hii ya umbo la ndani kuonekana na mofimu ya nje ilibainika katika nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM, hasa mofimu za pili zinapochukua viambishi vya wingi. Mathalani, mtafiti atatumia nomino ambatani ‘mwanamke’ kama kiwakilishi cha nomino zilizoorodheshwa katika Jedwali 2.1 kuonesha namna umbo la ndani huonekana na mofimu ya nje. Nomino ambatani ‘mwanamke’ ina mofu mbili; *{mw}* na *{anamke}* na katika kuambisha nomino ambatani hii kisarufi katika hali ya wingi, mofu ya kwanza *{mw}* na mofu ya pili *{anamke}* huchukua viambishi vya wingi na kuwa *{w}* na *{anawake}*. Hali hii huonesha namna kiambishi *{m}* cha nomino ‘mke’ katika mofu ya pili {anamke} huonekana na mofu ya kwanza *{mw}* na hii ndiyo sababu ya nomino ambatani katika Jedwali 2.1 hukiuka Kanuni ya Kufuta

Mabano. Ili kutoa mwanga zaidi kuhusu nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM, sehemu ifuatayo 2.2 inaonesha maumbo mbalimbali ya nomino husika.

2.2 Uainishaji wa Nomino Ambatani

Lusekelo (2019) na Bisetto & Scalise (2005) wameainisha nomino ambatani katika makundi mbalimbali. Katika utafiti huu, mtafiti aliegemea uainishaji wa Selrik (1982), Mcmahon (2000), Gichuru (2010) na Katamba & Stonham (2019) ambapo aliziainisha nomino ambatani hizi thelathini katika makundi mawili; nomino ambatani sahili, na nomino ambatani changamani. Kulingana na wataalam hawa, nomino ambatani huwa na utaratibu ambao huwakilishwa kwa kanuni za jumla zinazoshabihiana na za unyambulishaji, na ambazo hazifungamani na mazingira maalum. Kanuni wanazorejelea hapa huwa na muundo wa A → B. Wanaendelea kusema kuwa nomino ambatani zenye maneno mawili huwa zinaundwa na kanuni A → BC ambapo neno A ni neno-unde la muungano wa maneno B na C. Uainishaji huu, ulifaa mtafiti katika kutambua maumbo ya nomino ambatani, yaani maneno yanayohusika katika uundaji wa nomino ambatani hizi.

2.3 Nomino Ambatani Sahili

Nomino ambatani sahili zilizopatikana kutokana na uchanganuzi wa data ya Jedwali 2.1 ni ishirini na nane. Mtafiti aliteua nomino ambatani kumi kama viwakilishi vya nomino hizi katika Jedwali 2.3 lifuatalo:

Jedwali 2.3: Nomino Ambatani Sahili

Nomino Ambatani (Umoja)	**Nomino Ambatani (Wingi)**
[**Mw** [ana**m**ke]]	[**wa** [ana**wa**ke]]
[**M** [ja**m**zito]]	[**wa** [ja**wa**zito]]
[**Ø [**raia **mw**ema]]	[**ø** [raia **w**ema]]
[**Mw** [alimu **m**kuu]]	[**w** [alimu **wa**kuu]]
[**Mw** [enye**ki**ti]]	[**w** [enye**vi**ti]]
[**M** [ke**mw**enza]]	[**wa**] [ke**we**nza]]
[**Mw** [ana**m**kaidi]]	[**w** [ana**wa**kaidi]]
[**M** [kaza**mw**ana]]	[**w** [akaza**wa**na]]
[**Mw** [ana**m**falme]]	[**w** [ana**wa**falme]]
[**Mw** [ana**m**potevu]]	[**w** [ana**wa**potevu]]

Nomino ambatani sahili ni aina za nomino ambazo huzingatia idadi ya maneno yanayotumiwa katika mchakato wa uundaji wa nomino hizi. Aina hizi za nomino huundwa na vijenzi viwili tu na huwa na sharti ambalo hufuatwa katika utaratibu wa uundaji wake ambapo lazima maneno yawe mawili (Bencez, 2006; Kahigi, 2007; Tarasova, 2013). Katamba & Stonham (2019) wanaeleza kuwa katika mchakato wa kuambatisha aina hizi za nomino, lazima maneno ambatani yaoane, yaani yawe na unasaba wa kisemantiki.

Kwa mujibu wa Kanuni ya Mzunguko Kamili wa Mofolojia Leksia, vijenzi (maumbo yanayojengwa) katika nomino ambatani huwa vimeundwa katika mzunguko wa kwanza kabla ya kupitishwa katika ngazi ya pili ambapo huambatishwa kwa kutumia kaida za lugha inayohusika (Kiparsky, 1982; Mcmahon, 2000). Katika mchakato wa uundaji wa nomino ambatani, sheria za fonolojia na mofolojia hushirikiana katika kila ngazi ya mzunguko kabla ya kupitishwa katika mzunguko unaofuatia na uhusiano huu hurejelea kiwango maalum cha ngazi ya kileksika. (Rasim, 2020, Booij 2014, Gichuru 2010, Macmahon 2000, Kiparsky, 1982). Kuonesha kile kinachotokea katika kila ngazi, Jedwali 2.4 lifuatalo linadhihirisha uhusiano wa fonolojia na mofolojia kupitia badiliko la vokali /u/ kuwa nusu vokali /w/, badiliko la kudondosha irabu /u/

ikitanguliwa na konsonanti, na vipashio vya kifonolojia vinavyotumika kuunda vipashio vya kimofolojia.

Jedwali 2.4: Uhusiano wa Fonolojia na Mofolojia



Ngazi ya kwanza katika Jedwali 2.4 huhusika na kuonesha mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea wakati kiambishi kinapochopekwa kwenye mzizi wa nomino; mathalan, nomino *mwana* na *mke*. Nomino *mwana* hupitia badiliko la kifonolojia ambapo vokali /u/ huwa nusu vokali /w/ yaani, *{mu + ana}* kuwa *mwana*. Pia nomino *mke* hupitia badiliko la kifonolojia ambapo vokali /u/ hudondoshwa ikitanguliwa na konsonanti; *{mu + ke}* kuwa *mke*. Kinachodhihirika katika ngazi hii, ni kuwa mofimu ya pili ya nomino ambatani ‘mwanamke’ yaani *{anamke}* huchukua kiambishi {m-} na {mw} ambayo katika hali ya wingi huchukua mofu {w} na hii huwa ndiyo sababu za nomino hizi kukiuka KKM hasa mofimu ya pili *{anawake}* inapochukua kiambishi cha wingi.

Katika ngazi ya pili vipashio huambatishwa kuhakikisha kuwa nomino zinafuata kanuni ya lugha husika; *[[mwana] [mke]]*. Hii ndiyo hatua ambapo mabano ya katikati hufutwa na ngazi ya tatu huhusika na kuunganisha nomino mbili; *[[mwana][mke]]* kuwa *[mwanamke]* na kuhakikisha nomino ambatani iliyoundwa ina maana inayokubalika kisarufi. Kielelezo 2.4 kifuatacho kinadhihirisha uhusiano wa kimofolojia na kifonolojia katika uundaji wa nomino ambatani ‘mwanamke.’

Kielelezo 2.4: Uhusiano wa Kimofolojia na Kifonolojia

	Mofolojia	Fonolojia	Mofolojia	Fonolojia
Shina		mwana		mke
		↓		↓
Ngazi 1	[[mu + ana]]	⟷ [[mu + ana]]	[[mu + ke]]	⟷ [[mu + ke]]
		↓		↓
Ngazi 2		[[mwana]]		[[mke]]
		↓		
Ngazi 3		$[[\text{mwana}]_N [\text{mke}]_N]]_N$ ⟶ mwanamke		

Kielelezo 2.4 kinadhihirisha uhusiano wa sheria za kimofolojia na kifonolojia katika uundaji wa nomino ambatani, ambapo ngazi ya kwanza inaonesha viambajengo vya nomino ambatani husika. Katika ngazi ya pili nomino *{mu + ana}* na *{mu + ke}* hupitia badiliko la kifonolojia ambapo vokali /u/ katika *{mu + ana}* huwa nusu vokali /w/ kuwa *mwana* na kwa upande mwingine vokali /u/ katika *{mu + ke}* hudondoshwa kuwa *mke*, na ngazi ya tatu inaonesha neno lililo kamili na mabano yote hubomolewa kuashiria mwisho wa uundaji wa nomino ambatani husika.

2.3.1 Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Nomino

Nomino ambatani sahili za umbo la nomino na nomino ambazo mtafiti alibaini kutokana na data ya Jedwali 2.1 ni kama zifuatazo katika Jedwali 2.5:

Jedwali 2.5: Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Nomino

Nomino Ambatani	**Umoja**	**Wingi**
Mwanamke	[**mw** [ana**m**ke]]	[**w**] [ana**wa**ke]]
Mwanamfalme	[**mw** [ana**m**falme]]	[**w** [ana**wa**falme]]
Mkazamjomba	[**m** [kaza**m**jomba]]	[**wa** [kaza**wa**jomba]]
Msikilizaji mtazamaji	[**m** [sikilizaji **m**tazamaji]]	[**wa** [sikilizaji **wa**tazamaji]]
Mtungamziki	[**m** [tunga**m**ziki]]	[**wa** [tunga**mi**ziki]]
Msaidizi mshauri	[**m** [saidizi **m**shauri]]	[**wa** [saidizi **wa**shauri]]
Mkazamwana	[**m** [kaza**mw**ana]]	[**wa** [kaza**w**ana]]

Jedwali 2.5 linadhihirisha nomino ambatani ambazo huwa na umbo ambalo nomino mbili huunganishwa kuunda neno jipya, na ambalo huwakilisha dhana moja. Kanuni ya kuunganisha aina hizi za nomino ni kama ifuatayo:

$$[Y_1]_N + [Y_2]_N \rightarrow [[Y]_N\ [Y]_N]$$

Katika kanuni hii, nomino Y_1 na nomino Y_2 huunganishwa kuunda neno jipya.

Mtafiti alitumia nomino ambatani ‘mkazamjomba’ kueleza utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani za Jedwali 2.5. Katika hatua ya kwanza viambishi huchopekwa katika mizizi ya nomino *mkaza* na *mjomba* kama ifuatavyo; $[[[m]_{kia.}[kaz]_{\ mzizi\ }][a]]_{kiishio}$ $[[m]_{kia.}[jomba]]_{mzizi}$. Hatua ya pili huhusisha kuambatisha viambishi katika mizizi [kaz] na [jomba] kuwa; $[[mkaza]_N\ [mjomba]]_N$. Hii ndiyo hatua ambapo mabano ya katikati hufutwa. Hatua ya tatu huhusisha kuunganisha pamoja nomino hizi kuunda nomino ambatani *[mkazamjomba]*, na hatua ya mwisho huwa ni hatua ya kubomoa mabano kama inavyodhihirika katika nomino ambatani *mkazamjomba*. Nomino ambatani *mkazamjomba* inapochukua kiambishi cha wingi huwa *[wa*

[kazawajomba]] ilhali tunajua kuwa Kanuni ya Kufuta Mabano huruhusu mofimu ya kwanza *{m}* kuchukua kiambishi cha wingi; ***[wa [kazamjomba]]*. Mofimu ya pili *{kazamjomba}* inapochukua kiambishi cha wingi na kuwa *{kazawajomba}* inadhihirisha ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano.

Jedwali 2.5 linathibitisha kuwa nomino zote katika kikundi hiki huchukua utaratibu wa [wingi + Y_1] + [wingi + Y_n] ambao ni kinyume na Kanuni ya Kufuta Mabano ambayo inaruhusu urejeleaji nyuma wa mofimu ya kwanza pekee. Kwa mujibu wa Pesetsky (1979), Kanuni ya Kufuta Mabano huwa na mkabala ambao unaruhusu fonolojia kurejelea mipaka iliyotolewa na ujenzi wa mofolojia nje, lakini hairuhusu kurejelea muundo wa ndani wa neno zima. Mawazo ya Pesetsky (keshatajwa) yanaoana na ya Kiparsky (1982) ambaye pia anasisitiza kuwa mabano ya ndani yafutwapo mwisho wa kiwango cha leksia, hayawezi kuathiriwa na sheria za fonolojia ya mzunguko. Maoni ya Pesetsky (1979) na Kiparsky (1982) yanatofautiana na Orgun & Inkelas (2000) ambao wanaona kuwepo kwa sababu za kutazama tena ufutaji mabano. Katika utafiti wao wanaeleza sababu za baadhi ya nomino kukubali kutokea kwa mabadiliko katikati ya neno baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa. Matokeo ya tafiti za Pesetsky (1979), Kiparsky (1982) na Orgun & Inkelas (2000) yalisaidia mtafiti katika kujua utaratibu unaohusika katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili zilizochanganuliwa na namna zinavyoghairi Kanuni ya Kufuta Mabano.

2.3.2 Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Kivumishi

Nomino ambatani hizi huundwa kutokana na kuunganisha nomino na kivumishi kuunda neno jipya. Maumbo ya nomino na kivumishi huwa ya aina mbili:

2.3.2.1 Umbo la Nomino kutangulia Kivumishi

Maumbo haya yanahusisha uundaji wa nomino ambatani ambapo nomino hutangulia kivumishi. Aina hiii ya maumbo huwa na utaratibu unaozingatiwa kama ifuatavyo:

$[Y_1]_N + [Y_2]_V \rightarrow [[Y]_N [Y]_V]_N$

Ufafanuzi wa utaratibu huu: Nomino Y_1 huunganishwa na kivumishi Y_2 kuunda nomino mpya.

Nomino ambatani zinazokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano katika kategoria hii ni kama zifuatazo katika Jedwali 2.6.

Jedwali 2.6: Maumbo ya Nomino kutangulia Kivumishi

Nomino Ambatani	**Umoja**	**Wingi**
Raia mwema	[ø [raia **m**wema]]	[ø [raia **w**ema]]
Mjamzito	[**m** [jamzito]]	[**wa** [ja**wa**zito]]
Mwalimu mkuu	[**mw** [alimu **m**kuu]]	[**w** [alimu **wa**kuu]]
Mwanamkaidi	[**mw** [ana**m**kaidi]]	[**w** [ana**wa**kaidi]]
Kiunga mwana	[**ki** [unga **m**wana]]	[**vi** [unga **w**ana]]
Baba mkubwa	[ø [baba **m**kubwa]]	[ø [baba **wa**kubwa]]
Baba mdogo	[ø [baba **m**dogo]]	[ø [baba **wa**dogo]]
Bwana mdogo	[ø [bwana **m**dogo]]	[ø [bwana **wa**dogo]]

Nomino ambatani zilizoorodheshwa katika Jedwali 2.6 ni za umbo la nomino kutangulia kivumishi. Mofimu ya pili ya nomino ambatani hizi huwa na vivumishi ambavyo katika mazingira ya kawaida huchukua mofu za wingi. Mathalan; *mwema → wema, mzito → wazito, mkuu → wakuu, mkaidi → wakaidi, mwana → wana, mkubwa → wakubwa,* na *mdogo → wadogo*. Vivumishi hivi vinapoambatishwa na nomino huunda nomino ambatani. Baada ya nomino ambatani hizi kuambatishwa kama vile ‘baba mdogo,’ Kanuni ya Kufuta Mabano hairuhusu fonolojia kurejelea umbo la ndani la neno husika yaani mofimu ya pili {baba mdogo}. Hivyo basi, uwekaji wazi wa mofimu hii kwa kuiambisha katika hali ya wingi kuwa {baba

wadogo} inadhihirisha ukiukaji wa KKM. Hali hii hutokea katika nomino ambatani zote katika Jedwali 2.6 kwa kuwa vivumishi vyote katika mofimu za pili za nomino ambatani hizi huchukua mofu za wingi ili kuleta maana za kisarufi.

2.3.2.2 Nomino Ambatani za Umbo la Kivumishi kutangulia Nomino

Nomino ambatani hizi ni tofauti na mifano iliyodhihirishwa katika Jedwali 2.6 kwa kuwa kivumishi hutangulia nomino. Utaratibu unaohusika ni kama ufuatao:

$[Y_1]_V + [Y_2]_N \rightarrow [[Y]_V [Y]_N]_N$

Ufafanuzi wa utaratibu huu: Kivumishi Y_1 huunganishwa na nomino Y_2 kuunda nomino mpya.

Jedwali 2.7 lifuatalo linadhihirisha aina za muundo huu wa nomino ambatani ambazo zinaghairi Kanuni ya Kufuta Mabano.

Jedwali 2.7: Maumbo ya Kivumishi kutangulia Nomino

Nomino Ambatani	**Umoja**	**Wingi**
Mwenyekiti	[**mw** [enye**ki**ti]]	[**w** [enye**vi**ti]]
Mkuu mwenzio	[**m** [kuu **m**wenzio]]	[**wa** [kuu **w**enzio]]

Nomino ambatani katika kundi hili zimeundwa kutokana na kuambatisha vivumishi na nomino. Mofimu ya pili ya nomino ambatani hizi zina nomino ambazo ni; ‘kiti’ na ‘mwenzio.’ Nomino hizi katika mazingira ya kawaida huchukua viambishi vya *wingi; kiti → viti* na *mwenzio → wenzio*. Katika mchakato wa kuambisha kisarufi hali ya wingi nomino ambatani ‘mwenyekiti’ na ‘mkuu mwenzio’ kwa kuongozwa na Kanuni ya Kufuta Mabano, nomino ambatani hizi huchukua viambishi vya wingi katika mofimu ya kwanza pekee yaani, mwenyekiti → *wenyekiti, na mkuu mwenzio → *wakuu mwenzio. Hali hii huleta mgongano wa kiidadi ambao husababishwa na vijenzi vya nomino ambatani hizi kutokuwa na maana ya kisarufi. Kuondoa

mgongano wa kiidadi huu, nomino ambatani hizi hukiuka KKM kwa kuruhusu nomino zilizopo katika mofimu za pili kuchukua mofu za wingi mathalan; *mwenyekiti → wenyeviti* na *mkuu mwenzio → wa kuu wenzio*.

2.3.3 Nomino Ambatani za Umbo la Nomino na Kielezi

Nomino ambatani hizi huhusisha kuunganishwa kwa nomino na kielezi ili kuunda neno jipya. Nomino hizi huwa na utaratibu ufuatao:

$$[Y_1]_N + [Y_2]_E \rightarrow [[Y]_N [Y]_E]_N$$

Ufafanuzi wa utaratibu huu: nomino Y_1 huunganishwa na kielezi Y_2 kuunda nomino mpya.

Maneno katika kategoria hii yanayokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ni kama yafuatayo katika Jedwali 2.8:

Jedwali 2.8: Maumbo ya Nomino na Kielezi

Nomino Ambatani	**Umoja**	**Wingi**
Kirai kielezi	[**ki** [rai **ki**elezi]]	[**vi** [rai **vi**elezi]]
Kirai kitenzi	[**ki** [rai **ki**tenzi]]	[**vi** [rai **vi**tenzi]]
Kirai kiunganishi	[**ki** [rai **ki**unganishi]]	[**vi [**rai **vi**unganishi]]
Kirai kivumishi	[**ki** [rai **ki**vumishi]]	[**vi** [rai **vi**vumishi]]

Mofimu ya pili katika nomino ambatani hizi huwa na vielezi ambavyo katika mchakato wa uambishaji katika hali ya wingi huchukua viambishi vya wingi kama ifuatavyo: *kielezi → vielezi, kitenzi → vitenzi, kiunganishi → viunganishi,* na *kivumishi → vivumishi*. Kinyume na inavyodhihirika katika Jedwali 2.8, Kanuni ya Kufuta Mabano huruhusu uambishaji wa kisarufi kutokea katika mofimu za kwanza pekee yaani; *kirai kielezi → *virai kielezi, kirai kitenzi → *virai kitenzi, kirai kiunganishi → *virai kiunganishi, na kirai kivumishi → *virai kivumishi*. Urejeleaji wa fonolojia katika mofolojia ya nje ya nomino ambatani hizi, huzua maneno ambayo

katika lugha ya Kiswahili hayana umbo sahihi, na kuzifanya nomino ambatani hizi kuwa sahihi kisarufi inalazimu kukiuka KKM kama inavyodhihirika katika Jedwali 2.8 ambapo nomino ambatani katika kundi hili huchukua viambishi vya wingi katika mofimu za kwanza na za pili katika mofu husika.

2.4 Nomino Ambatani Changamani

Hizi ni aina za nomino ambatani ambazo huundwa na zaidi ya maneno mawili ambayo huambatishwa ili kuunda neno changamani moja. Kulingana na data iliyochanganuliwa, mtafiti alipata aina tatu za nomino ambatani changamani zinazokiuka KKM kama ifuatavyo katika Jedwali 2.9:

Jedwali 2.9: Nomino Ambatani Changamani

Nomino Amabatani	**Umoja**	**Wingi**
Utiwamgongo	[**ø** [utiwa**m**gongo]]	[**ø** [utiwa**mi**gongo]]
Mwanamkendege	[**m**wa [ana**m**kendege]]	[**w** [ana**wa**kendege]]
Mwanawamwana	[**mw** [anawamwana]]	[**w** [ana**wa**wana]]

Hizi ni aina za nomino ambatani ambapo maneno matatu au zaidi huunganishwa kuunda nomino ambatani. Mtafiti alitumia nomino ambatani ‘mwanamkendege’ kama kiwakilishi cha nomino zilizoorodheshwa katika Jedwali 2.9 kueleza utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani hizi. Utaratibu unaohusika ni kama ufuatao:

$$[[mw]_{kia.}\ [ana]_{mzizi}]_N + [m]kia\ [mke]_{mzizi}]_N + [ndege]_{mzizi}]_N \rightarrow [mwanamkendege]_N$$

Neno hili linapoambishwa kisarufi katika hali ya wingi huwa *wanawakendege*, hali ambayo inadhihirisha mabadiliko katikati mwa mofimu *[anamkendege]* na hivyo basi, hali hii hukiuka KKM ambayo hairuhusu urejeleaji nyuma baada ya mabano kufutwa.

2.5 Mchakato wa Uambishaji Kisarufi wa Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM

Kutoa mwanga kuhusu mchakato huu, mtafiti alilinganisha uundaji wa nomino ‘mwanamgambo’ na ‘mkazamwana’ ili kueleza uambishaji kisarufi hatua kwa hatua:

$Y_1 \quad + \quad Y_2 \quad \rightarrow \quad [[Y_1] \quad [Y_2]]_N \quad \rightarrow \quad [Y_1Y_2]_N$

$[[mw]_{kia.}[ana]_{mzizi}+[[m]_{kia.}[gambo]_{mzizi}]_N \rightarrow [[mwana][mgambo]]_N \rightarrow [mwanamgambo]_N$

Hatua 1 Hatua 2 Hatua 3

Nomino ambatani ‘mwanamgambo’ inapoundwa na kufikia hatua ya 3 huwa na mofimu mbili; {mw} na {anamgambo} kinyume na ilivyokuwa katika hatua ya 1 ambapo ilikuwa na mofimu nne, yaani $\{mw\}_{kia.}\ \{ana\}_{mzizi} + \{m\}_{\ kia.}\ \{gambo\}_{mzizi}\}$. Nomino ambatani hii katika uambishaji kisarufi hukubali urejeleaji wa mofu ya kwanza yaani, *wanamgambo*. Nomino ambatani *mkazamwana* kwa upande mwingine ina utaratibu ufuatao:

$[[m]_{kia.}[kaza]_{mzizi}+[[m]_{kia.}\ [ana]_{mzizi}]_N \rightarrow [[mkaza][mwana]]_N \rightarrow [mkazamwana]_N$

Uambishaji kisarufi wa nomino ambatani *mkazamwana* katika hali ya wingi huwa *wakazawana* ilhali tunajua nomino ambatani hii katika umoja ina mofu mbili, yaani {m} na {kazamwana}. Kutokana na nomino ambatani zilizoorodheshwa katika sura hii, ni ithibati tosha ya kuwepo kwa nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM na hivyo basi, lengo la kudhihirisha nomino ambatani zinazokiuka KKM na maumbo yake yaliafikiwa.

2.6 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM. Ili kuafikia lengo la kudhihirisha nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka

KKM na maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM, utafiti huu uliongozwa na mihimili miwili, yaani mhimili wa Kanuni ya Kufuta Mabano na Kanuni ya Mzunguko Kamili. Mihimili hii ilitumikizwa katika kueleza utaratibu unaohusika katika uundaji wa nomino ambatani na namna ambavyo nomino hizi hukiuka utaratibu huu hasa pale zinapoambishwa kisarufi katika wingi, hali ambayo husababisha urejeleaji nyuma baada ya viambajengo mbalimbali kuunganishwa na mabano kubomolewa.

Mtafiti aliziainisha nomino ambatani thelathini zinazokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano katika makundi mawili yaani, nomino ambatani sahili (ishirini na nane) na nomino ambatani changamani (mbili). Katika kitengo cha nomino ambatani sahili ziliainishwa pia katika makundi matatu; nomino ambatani zenye umbo la nomino na nomino, nomino ambatani zenye umbo la nomino na kivumishi ambazo pia zilianishwa katika makundi mawili (nomino ambatani zenye umbo la nomino kutangulia kivumishi, na kivumishi kutangulia nomino), na nomino ambatani za umbo la nomino na kielezi. Nomino ambatani changamani zilizopatikana kutokana na data ya Jedwali 2.1 zilikuwa tatu. Pia mtafiti alieleza mchakato wa uambishaji wa kisarufi wa nomino ambatani zinazokiuka KKM.

Sura hii kwa muhtasari imeshughulika na kueleza jinsi baadhi za nomino ambatani za Kiswahili hukiuka KKM kwa kuchukua utaratibu huu [wingi + Y_1] + [wingi + Y_n] mathalan; ***m****kaza****m****wana* → ***w****aka**za****w****ana*. Utaratibu ambao ni kinyume cha Kanuni ya Kufuta Mabano kwani kanuni hii hairuhusu aina ya urejeleaji nyuma baada ya mabano kufutwa, na iwapo kutakuwa na urejeleaji nyuma hufuata utaratibu huu [wingi + Y_1] + [Y_n] kama inavyojitokeza katika nomino ambata; ***mw****anamgambo* → ***w****anamgambo*. Mwisho mtafiti alibaini uondoaji wa shadda kutoka neno la kwanza la nomino

ambatani na upachikaji upya wa shadda ya msingi katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno ambatani husika hutokea. Sura ya Tatu ifuatayo imeshughulika na sababu za baadhi za nomino ambatani kukiuka na kutokiuka KKM wakati zinapoambishwa katika hali ya wingi.

SURA YA TATU

SABABU ZA KUKIUKA NA KUTOKIUKA KANUNI YA KUFUTA MABANO

3.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki kwa kuongozwa na mhimili wa KKM na Kanuni ya Mzunguko Kamili. Kujibu swali hili la utafiti, mtafiti alichanganua nomino ambatani sitini yaani thelathini zinazokiuka na thelathini zisizokiuka KKM. Nomino ambatani hizi ziliainishwa katika makundi mawili na kuzitolea sababu ambazo husababisha kukiuka au kutokiuka KKM.

3.1 Sababu za Baadhi za Nomino Ambatani Kukiuka KKM

Data ya nomino ambatani za Kiswahili ambazo hukiuka KKM, kama ilivyokwisha kudhihirishwa katika Sura ya Pili, ni nomino ambatani thelathini. Kutokana na uchanganuzi wa data ya Jedwali 2.1, mtafiti aliweza kubaini sababu ambazo husababisha mabadiliko kutokea katikati mwa nomino ambatani hizi baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa kuwa: mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana na mofu ya kwanza, na muktadha wa matumizi ya nomino ambatani.

3.1.1 Mofu ya Pili Kuonekana na Mofu ya Kwanza

Kutokana na uchanganuzi wa data ya utafiti huu, mtafiti aliziainisha nomino ambatani hizi kwa kuelekezwa na ngeli zinazopatikana ili kudhihirisha uwepo wa sifa hii ya mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana na mofu ya kwanza. Jedwali 3.1 lifuatalo linadokeza nomino ambatani zenye mofu ya pili kuonekana na mofu ya kwanza:

Jedwali 3.1: Mofu ya Pili Kuonekana na Mofu ya Kwanza

Nomino ambatani (Ngeli ya A-WA)	**Uchukuaji wa Wingi kulingana na KKM**	**Uchukuaji wa wingi kwa Kukiuka KKM**
[**Mw** [ana**m**ke]]	*[**w** [ana**m**ke]]	[**w** [ana**wa**ke]]
[**Mw** [ana**m**kaidi]]	*[**w** [ana**m**kaidi]]	[**w** [ana**wa**kaidi]]
[**Mw** [ana**m**potevu]]	*[**w** [ana**m**potevu]]	[**w** [ana**wa**potevu]]
[**Mw** [ana**m**kendege]]	*[**w** [ana**m**kendege]]	[**w** [ana**wa**kendege]]
[Mw [ana**m**wali]]	*[**w** [ana**mw**ali]]	[**w** [ana**w**ali]]
[**M** [ja**m**zito]]	*[**wa** [jamzito]]	[**wa** [ja**wa**zito]]
[**M** [saidizi **m**shauri]]	*[**wa** [saidizi **m**shauri]]	[**wa** [saidizi **wa**shauri]]

Sababu za mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana na mofu ya kwanza ni: upatanisho wa kisarufi, mgongano wa idadi hasa nomino zinapoambatishwa kisarufi katika hali ya wingi, na mvutano unaotokea katika baadhi ya nomino ambapo neno katika mofu ya pili huwa na mofu ambayo ni tofauti na mofu ya kwanza lakini kunatokea hali ya wingi. Mtafiti amezieleza sababu hizi za kuonekana kwa mofu ya pili na mofu ya kwanza moja baada ya nyingine.

3.1.1.1 Upatanisho wa Kisarufi

Nomino ambatani zilizoorodheshwa katika Jedwali 3.1 zinadhihirisha kuwepo kwa sifa ya mofu ya pili ya nomino ambatani kuwa na viambishi vinavyoonekana na mofu ya kwanza. Mathalan mtafiti atatumia nomino ambatani ‘mwanamke’ kuonesha namna hali hii hutokea katika mchakato mzima wa uambishaji kisarufi wa nomino ambatani hizi.

Nomino ambatani ‘mwanamke’ ina mofu mbili yaani; *{mw}* na *{anamke}*. Nomino ambatani hii inapoambishwa kisarufi katika hali ya wingi mofu ya kwanza huchukua kiambishi cha wingi {w} na vilevile, mofu ya pili huchukua kiambishi cha wingi {wa} katika nomino ‘mke’ iliyoambatishwa katika mzizi {ana} kuwa *{anawake}*. Katika nomino ambatani *[mw [anamke]]*, mofu ya pili {anamke} inaonekana na mofu ya kwanza hasa pale ambapo kiambishi {m} katika nomino ‘mke’ kinapochukua

kiambishi {wa} ili kuleta maana ya kisarufi. Kuonekana kwa mofu ya pili ya nomino ambatani na mofu ya kwanza husababishwa na upatanisho wa kisarufi ili kuleta neno lililo na maana kubalifu.

Upatanisho wa kisarufi unaorejelea hapa ni namna vipashio mbalimbali vya nomino ambatani vinavyochukuana na kukubaliana ili kuunda neno lenye maana (Habwe & Karanja, 2004). Maoni ya Habwe & Karanja (keshatajwa) yanaoana na yale ya Katamba & Stonham (2019) ambao wanasema kuwa lazima umbo la neno linaloambatishwa kupata neno ambatani lioane, yaani liwe na unasaba wa kisemantiki, lilete maana. Wanachoashiria Katamba & Stonham (keshatajwa) ni uundaji wa nomino ambatani zilizo na maana sahihi kisarufi. Kwa kuzingatia KKM, nomino ambatani ‘mwanamke’ katika kuiambatisha kisarufi hali ya wingi inastahili kuwa **wanamke*, hali ambayo huleta neno lisilokubalika kisarufi. Kuondoa hali hii, nomino ambatani ‘mwanamke’ hughairi KKM kwa kuruhusu mabadiliko kutokea katikati mwa nomino ambatani hii na kuwa ‘wanawake.’ Mabadiliko haya hutokea katika nomino ambatani zilizoorodheshwa katika Jedwali 3.1 zinapochukua viambishi vya wingi katika mofu ya kwanza na ya pili ya nomino ambatani ili kuleta neno lililo na maana kamili. Kutoa ufafanuzi zaidi wa mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana na mofu ya kwanza mtafiti alibaini kutokea kwa mgongano wa kiidadi katika nomino ambatani hizi.

3.1.1.2 Mgongano wa Kiidadi wa Nomino Ambatani za Kiswahili

Jedwali 3.2 lifuatalo linadhihirisha nomino ambatani za ngeli A-WA na KI-VI zinazodokeza mgongano wa kiidadi wa nomino ambatani za Kiswahili:

Jedwali 3.2: Nomino Ambatani za Ngeli A-WA na KI-VI

Nomino Ambatani (Ngeli A-WA na KI-VI	**Uchukuaji wa Wingi Kulingana na KKM**	**Uchukuaji wa Wingi kwa Kukiuka KKM**
[**Mw** [enye**ki**ti]]	*[**w** [enye**ki**ti]]	[**w** [enye**vi**ti]]
[**M** [kaza**m**jomba]]	*[**wa** [kaza**m**jomba]]	[**wa** [kaza**wa**jomba]]
[**M** [hariri **m**kuu]]	*[**wa** [hariri **m**kuu]]	[**wa** [hariri **wa**kuu]]
[**M** [kuu **mw**enzio]]	*[**wa** [kuu **mw**enzio]]	[**wa** [kuu **w**enzio]]
[**Ki** [rai **ki**unganishi]]	*[**vi** [rai **ki**unganishi]]	[**vi** [rai **vi**unganishi]]
[**Ki** [rai **ki**tenzi]]	*[**vi** [rai **ki**tenzi]]	[**vi** [rai **vi**tenzi]]
[**Ki** [rai **ki**vumishi]]	*[**vi** [rai **ki**vumishi]]	[**vi** [rai **vi**vumishi]]
[**Ki** [rai **ki**elezi]]	*[**vi** [rai **ki**elezi]]	[**vi** [rai**vi**elezi]]

Nomino ambatani zilizopachikwa alama ya kinyota katika Jedwali 3.2 zinadhihirisha mgongano wa idadi hasa zinapozingatia KKM na Kanuni ya Mzunguko Kamili katika uambishaji kisarufi katika hali ya wingi. Nomino ambatani hizi huwa na viambishi vinavyowakilisha idadi, yaani umoja na wingi. Mofu ya kwanza katika nomino ambatani hizi huchukua viambishi vya wingi ambavyo huathiri neno lililopo katika mofu ya pili ya nomino ambatani kwa kuchukua pia kiambishi cha wingi.

Mtafiti anachoeleza hapa ni kile Mpiranya (2015) na Habwe & Karanja (2004) wanasema kuwa kiambishi cha kwanza cha nomino ndicho huamua ngeli ya viambishi vya wingi vya nomino husika. Maoni haya yanaoana na yale ya Lusekelo (2019) ambaye anasema kuwa viambishi vya nomino ya kushoto katika mwambatano huamua mifumo ya makubaliano katika virai, vitenzi, na nomino na katika muktadha wa utafiti huu ni makubaliano ya viambajengo vya nomino ambatani. Mtafiti anakubaliana na wataalam hawa kuhusu kiambishi cha kwanza kuamua ngeli na viambishi vya nomino ambatani husika. Hata hivyo, nomino ambatani zilizopachikwa alama ya kinyota katika Jedwali 3.2 hazifuati utaratibu huu kwa kuwa mofu ya kwanza ndiyo pekee huchukua viambishi vya wingi, hali ambayo huleta mgongano wa kiidadi hasa nomino ambatani hizi zinapochukua viambishi vya wingi. Mathalan mtafiti

atatumia nomino ambatani ‘mkuu mwenzio’ na ‘kirai kiunganishi’ kama viwakilishi vya nomino ambatani za Jedwali 3.2 kueleza namna ambavyo mgongano wa kiidadi hutokea hasa zinapochukua viambishi vya wingi katika mofu ya kwanza pekee.

Nomino ambatani ‘mkuu mwenzio’ na ‘kirai kiunganishi’ zinapoambishwa kisarufi katika hali ya wingi kwa kuelekezwa na Kanuni ya Kufuta Mabano huwa: **wakuu mwenzio* na **virai kiunganishi*. Nomino hizi huwa hazina upatanisho wa kisarufi sahihi kwani kunatokea mgongano wa kiidadi ambapo neno la kwanza linarejelea hali ya wingi ilhali la pili linarejelea hali ya umoja. Hali hii ya mgongano wa kiidadi hulazimu kutokea ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano ambapo nomino ambatani hizi huchukua viambishi vya wingi katika mofu zote za nomino ambatani husika na kuwa: ‘wakuu wenzio’ na ‘virai viunganishi’ na hali hii hudhihirisha upatanisho wa kisarufi sahihi.

Kinachotokea katika nomino ambatani za Jedwali 3.2 ni kuwa mofu ya kwanza ya nomino ambatani huamua kiambishi cha wingi katika viambajengo vyake. Hali hii ya mofu ya kwanza katika nomino ambatani kuchukua na kuamua viambishi vya wingi vinavyofanana haitokei katika nomino ambatani zote. Jedwali 3.3 lifuatalo linadhihirisha baadhi ya nomino ambatani za ngeli A-WA na KI-VI ambazo mofu ya kwanza na ya pili zinatofautiana lakini zinachukua viambishi vya wingi. Nomino ambatani hizi huwa na mofu kapa katika kiambishi awali lakini hukubali mabadiliko kutokea katika mofu ya pili kama ifuatavyo katika Jedwali 3.3:

Jedwali 3.3: Mofu Tofauti Zinazochukua Viambishi vya wingi

Nomino Ambatani (Ngeli A-WA na KI-VI)	**Umoja**	**Wingi**
Raia mwema	[**ø** [raia **mw**ema]]	[**ø** [raia **w**ema]]
Baba mdogo	[**ø** [baba **m**dogo]]	[**ø** [baba **wa**dogo]]
Bwana mdogo	[**ø** [bwana **m**dogo]]	[**ø** [bwana **wa**dogo]]
Baba mkubwa	[**ø** [baba **m**kubwa]]	[**ø** [baba **wa**kubwa]]

Nomino ambatani za ngeli ya A-WA yaani *[ø [raia mwema]]*, *[ø [baba mdogo]]*, *[ø [bwana mdogo]]* na *[ø [baba mkubwa]]* huwa na mofu kapa katika mofu za kwanza. Mtafiti anachorejelea kuwa mofu kapa ni kile Habwe & Karanja (2004) wanachoeleza kuwa kipashio cha kidhahania kilichoundwa kwa madhumuni ya uchunguzi tu lakini hakijitokezi wazi. Nomino ambatani hizi zinapoambishwa kisarufi katika hali ya wingi huchukua viambishi vya wingi katika mofu ya pili pekee na kuwa *[ø [raia wema]]*, [ø *[baba wadogo]]*, *[ø [bwana wadogo]]*, na *[ø [baba wakubwa]]*. Hali hii ya kuambisha kisarufi mofu ya pili katika hali ya wingi hutokea kwa sababu umbo kapa haliwezi kubainisha kama neno la kwanza lipo katika wingi au umoja. Kwa sababu hiyo, inabidi lile la pili liwe katika wingi ili kuthibitisha idadi katika neno husika.

3.1.1.3 Mvutano Unaotokea katika Nomino Ambatani za Kiswahili

Mtafiti alibaini pia sababu nyingine ya nomino ambatani hizi kukiuka KKM kuwa mvuto katika hali ya wingi. Mvuto katika hali ya wingi unaorejelea katika sehemu hii ni pale ambapo mofu za kwanza huathiri mofu za pili kuchukua viambishi vya wingi ili kuwa na umbo lililo sahihi kisarufi. Mathalan nomino za ngeli ya KI-VI: *[ki [ungamwana]] → [vi [ungawana]]*, na *[ki [takasa mkono]] → [vi [takasa mikono]]*. Mabadiliko haya pia hutokea katika nomino ambatani za ngeli LI-YA; *[ø [nenokuu]] → [ma [nenomakuu]]* na ngeli U-I; [*ø [utiwamgongo]] → [utiwamigongo]]* ambapo

neno la kushoto ndilo linalobeba uamilifu wa nomino husika na hukubali mabadiliko kutokea iwapo mofu ya pili ina neno linaloweza kuchukua mofu ya wingi.

Kinachodhihirika katika nomino ambatani zinazokiuka KKM ni uwekaji wazi wa umbo la ndani la neno kwa fonolojia. Orgun & Inkelas (2002) wanadai kuwepo kwa nadharia inayoweka wazi mofolojia ya ndani kwa fonolojia katika mchakato wa uundaji wa maneno. Maoni haya yanaoana na ya Cole (1995) ambaye anasema kuwa muundo wa ndani wa mofolojia ya neno lazima uonekane ili kupata athari za mzunguko kwa kuweka vizuizi katika vikoa vilivyoainishwa kimofolojia. Nomino ambatani hizi zinapoambishwa katika hali ya wingi hudhihirisha uwekaji wazi wa mofolojia ya ndani kwa fonolojia hata baada ya nomino ambatani hizi kuundwa kikamilifu.

Kwa mujibu wa Allen (1978), mofu ya kwanza katika neno zima huweza kuwekwa katika hali ya wingi bila kuingia katika mofu ya pili ya neno zima. Katika muktadha wa KKM, nomino ambatani hizi zinastahili kuchukua viambishi vya wingi katika mofu za kwanza za nomino ambatani. Hata hivyo imebainika hali hii ni tofauti, kwani nomino ambatani hizi zinakiuka kanuni hii, kwa kuchukua viambishi vya wingi katika mofu ya pili ya nomino ambatani husika. Maoni ya Allen (1978) yanatofautiana na Cole (1995) na Orgun & Inkelas (2002) ambao wanaona kuwa nomino ambatani hizi hukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano kutokana na kuonekana kwa kiambishi cha mofu ya pili ya nomino ambatani na mofu ya kwanza ili kupata upatanisho wa kisarufi, kuondoa mgongano wa kiidadi, na kuonesha mvutano wa wingi unaotokea katika mchakato wa kuambisha nomino ambatani hizi katika hali ya wingi. Maoni ya Orgun & Inkelas (keshatajwa} na Cole (1995) yanaoana na yale ya Hammond (1991) ambaye pia anasema kuwa mofu ya pili ya neno huonekana na mofu ya kwanza ya neno husika

na hili husababisha urejeleaji nyuma wa neno baada ya viambajengo mbalimbali kuunganishwa katika mchakato wa kuambisha kisarufi nomino ambatani za Kiswahili katika hali ya wingi.

3.1.2 Muktadha wa Matumizi ya Nomino Ambatani

Nomino ambatani zinazokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano zilizodhihirisha sifa ya kutegemea muktadha katika matumizi yao ni kama zifuatazo katika Jedwali 3.4:

Jedwali 3.4: Muktadha wa Matumizi ya Nomino Ambatani

Nomino Ambatani (Umoja)	**Uchukuaji wa Wingi Kulingana na KKM**	**Uchukuaji wa Wingi kwa Kiuka KKM**
Mwanamfalme	[**w** [ana**m**falme]]	[**w** [ana**wa**falme]]
Mwanawamwana	[**w** [anawa**m**wana]]	[**w** [anawa**w**ana]]
Kitakasa mkono	[**vi** [takasa **m**kono]]	[**vi** [takasa **mi**kono]]

Nomino ambatani katika Jedwali 3.4 zinachukua uambishaji kisarufi katika mofu ya kwanza pekee, hali ambayo Kanuni ya Kufuta Mabano inakubali. Hata hivyo, katika muktadha wa matumizi ya nomino ambatani hizi huwa kunazuka utata wa kimatumizi pale ambapo mofu ya pili ya nomino ambatani inaporejelea zaidi ya kitu au mtu mmoja. Mathalan nomino ambatani ‘wanamfalme’ katika muktadha wa kurejelea hali ya ‘mfalme’ kuwa na ‘wana’ wengi ni sawa, na hali hii huwa haikiuki Kanuni ya Kufuta Mabano.

Utata wa kimatumizi unazuka pale ambapo tunarejelea zaidi ya ‘mfalme’ mmoja, na hili husababisha mabadiliko katika mofu ya pili *{anamfalme}* kuwa *{anawafalme}* kama inavyojitokeza katika nomino ambatani *wanawafalme.* Nomino ambatani ‘vitakasa mkono,’ na ‘wanawamwana’ zinazua utata wa aina hii pale ambapo mofu ya pili inachukua kiambishi cha wingi ili kuleta dhana ya zaidi ya kitu kimoja

kinachoashiriwa kama inavyodhihirika katika nomino ambatani *kitasa mkono → vitakasa mikono* na *mwanawamwana → wanawawana*.

Ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika aina za nomino ambatani hizi, unaoana na mawazo ya Deda (2015) ambaye anaeleza pragmatiki kama usomaji wa lugha kwa mtazamo wa watumiaji, hasa uamuzi wanaofanya, vikwazo wanavyokutana navyo katika mwingiliano wa kijamii, na athari za matumizi yao ya lugha kwa washiriki wengine katika tendo la mawasiliano. Maoni ya Deda (2015) yanaoana na ya Jeffers & Lehiste (1979) ambao wanadai kuwa maana ya neno hutambuliwa kutokana na seti ya miktadha ambayo neno hilo hutokea. Tunakubalina na maoni ya Deda (keshatajwa) na Jeffers & Lehiste (1979) kuwa matumizi ya nomino ambatani hizi katika Jedwali 3.4 hutegemea muktadha wa matumizi yake, na hii ndiyo sababu nomino ambatani hizi hukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Sehemu 3.2 ifuatayo inashughulika na sababu za nomino ambatani zingine kuonekana kutokiuka KKM.

3.2 Sababu za Nomino Ambatani Zingine Kuonekana Kutokiuka KKM

Nomino ambatani zilizochanganuliwa kutoka *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) zisizokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ni thelathini. Mtafiti alibaini sababu za nomino ambatani hizi kuonekana kutokiuka KKM ambazo ni: mofu ya pili ya nomino ambatani kuwa na mofu kapa, na uundaji wa kimofolojia wa nomino ambatani usiopachika kiambishi cha wingi katika mofu ya kwanza. Sababu hizi zitaelezwa moja baada ya nyingine katika sehemu zifuatazo.

3.2.1 Mofu ya Pili ya Nomino Ambatani kuwa na Mofu Kapa

Katika uchanganuzi wa data iliyokusanywa na mtafiti, alibaini nomino ishirini na tatu ambazo zilidhihirisha sifa hii ya mofu ya pili ya nomino ambatani kuwa na mofu kapa.

Nomino ambatani hizi zilizigawa katika makundi manne, mtafiti akielekezwa na ngeli ambamo zinapatikana kama ifuatavyo: ngeli ya A-WA (nomino ambatani saba), ngeli ya KI-VI (nomino ambatani tano), ngeli ya LI-YA (nomino ambatani sita), na ngeli ya U-I (nomino ambatani tano). Kwa kuwa nomino ambatani zote katika makundi haya manne ya ngeli yanahusisha jambo hili la mofu ya pili kuwa na mofu kapa, nomino ambatani mbili kutoka kila kikundi zilitumiwa kama viwakilishi vya nomino ambatani zote ishirini na tatu kueleza sababu ya nomino ambatani hizi kuonekana kutokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano. Jedwali 3.5 lifuatalo linadhihirisha nomino ambatani zenye mofu ya pili kuwa na mofu kapa:

Jedwali 3.5: Mofu ya Pili kuwa na Mofu Kapa

Nomino Ambatani (Umoja)	**Nomino Ambatani (Wingi)**
[**M** [nadiswala]]	[**wa** [nadiøswala]]
[**Mw** [anasiasa]]	[**w** [anaøsiasa]]
[**M** [kundenyika]]	[**mi** [kundeønyika]]
[**M** [pilipilitao]]	[**mi** [pilipiliøtao]]
[**Ø** [anguotete]]	[**m** [anguoøtete]]
[**Ø** [punguzobei]]	[**ma** [punguzoøbei]]
[**Ki** [inilishe]]	[**vi** [iniølishe]]
[**Ki** [kosikazi]]	[**vi** [kosiøkazi]]

Jedwali 3.5 linadhihirisha nomino ambatani ambazo mofu za kwanza huchukua viambishi vya wingi ilhali nomino zilizo katika mofu za pili hazichukui viambishi vya wingi. Mofu za pili huwa na maneno ambayo katika mazingira ya kawaida hayachukui viambishi vya wingi katika mchakato wa kuambisha maneno haya katika hali ya wingi. Mathalan, *swala→ swala, siasa → siasa, nyika → nyika, tao → tao, tete → tete, bei → bei, lishe → lishe,* na *kazi → kazi* kwa kuwa nomino hizi zina mofu kapa.

Kinachobainika katika nomino za Jedwali 3.5, hasa mofu za kwanza zinapochukua viambishi vya wingi ni kile Gichuru (2010) na Kula (2012) wanarejelea kuwa kiambishi cha ngeli katika nomino ambatani huwa kichwa, yaani huamua kiambishi

cha wingi cha nomino husika. Nomino ambatani *[ø [anguotete]]* na *[ø [punguzobei]]* hazifuati utaratibu huu, kwa kuwa mofu za kwanza na za pili katika nomino ambatani hizi ni kapa na zinapoambishwa katika hali ya wingi, mofu za kwanza pekee ndizo huchukua viambishi vya wingi kuwa; *anguotete* → *manguotete* na *punguzobei* → *mapunguzobei*. Kwa mujibu wa Mpiranya (2015), aina za nomino hizi huwa na viambishi *{ø-li/ma-ya}* wakati zinapochukua viambishi vya wingi. Hata hivyo, hali hii haitokei katika nomino ambatani hizi, kwani mofu za kwanza pekee ndizo huchukua viambishi vya wingi, jambo ambalo ni la kushangaza.

Maneno katika mofu ya pili kutochukua viambishi vya wingi ni kile Carstens (1991) anaeleza kuwa kila kundi la nomino huwa linahusishwa na kiambishi fulani cha ngeli na muundo tofauti wa makubaliano yanayozalisha neno kubalifu. Maoni ya Carstens (1991) yanaona na yale ya Lusekelo (2019) ambaye anasema kuwa uamuzi juu ya makubaliano ya viambishi vya ngeli katika mchakato wa uambatani unategemea asili ya yaliyomo katika nomino husika. Makubaliano na uhusiano wa kisemantiki katika mchakato wa kuziambisha nomino ambatani hizi katika hali ya wingi ndiyo sababu za nomino ambatani hizi kuonekana kutokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ya Mofolojia Leksia.

3.2.2 Nomino Ambatani Zisizopachikwa Kiambishi cha Wingi katika Mofu ya Pili

Nomino ambatani zilizodhihirisha uundaji wa kimofolojia usiopachika kiambishi cha wingi katika mofu ya pili kutoka na uchanganuzi wa data iliyokusanywa ni kama zifuatazo katika Jedwali 3.6:

Jedwali 3.6: Mofu za Pili Zisizochukua Viambishi vya Wingi

Nomino Ambatani (Umoja)	**Nomino Ambatani (Wingi)**
[**M** [fumojike]]	[**mi** [fumoøjike]]
[**M** [sumenouta]]	[**mi** [sumenøouta]]
[**Ki** [ambajengo]]	[**vi** [ambaøjengo]]
[**Mw** [anamgambo]]	[**w** [anaømgambo]]
[**Ø** [spanaboi]]	[**ma** [spanaøboi]]
[**Ki [**banuaulimi]]	[**vi** [banuaøulimi]]
[**Ch** [amshakinywa]]	[**vi** [amshaøkinywa]]

Nomino ambatani katika Jedwali 3.6 zinadhihirisha kiambishi cha mofu ya pili kutoonekana na mofu ya kwanza na hii ndiyo hali halisi ya nomino ambatani hizi kutokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano na kuzingatia Kanuni ya Mzunguko Kamili ambayo hairuhusu ngazi za awali katika uundaji wa neno kurejelewa. Hali hii hutokea hasa pale ambapo katika mchakato wa uundaji kimofolojia wa nomino ambatani hizi, huwa hakutokei upachikaji wa kiambishi cha wingi katika nomino zilizopo katika mofu ya pili. Nomino zilizopo katika mofu ya pili ya nomino ambatani hizi huchukua viambishi vya wingi katika mazingira ya kawaida. Mathalan; *jike → majike, uta → nyuta, jengo → majengo, mgambo → migambo, boi → maboi, ulimi → ndimi*, na *kinywa → vinywa*. Hata hivyo, hali hii ni kinyume katika mofu ya pili ya nomino ambatani hizi katika Jedwali 3.6 kwani, nomino zilizopo katika mofu ya pili ya nomino ambatani hizi hazichukui kiambishi cha wingi katika uambishaji kisarufi kutokana na uzoefu wa kutopachika viambishi vya wingi katika mazungumzo ya kila siku kama inavyojitokeza katika nomino ambatani *[m [fumojike]]* kuwa *[mi [fumojike]]*.

Mofu kapa {ø} katika nomino ‘jike’ huwa {ma} katika hali ya wingi, lakini hali hii haitokei katika uambishaji kisarufi wa mofu {fumojike} na hili hudhihirisha uundaji

wa kimofolojia usiopachika kiambishi cha wingi katika mofu ya pili {fumojike} na hii ndiyo sababu ya nomino ambatani hizi kutokiuka Kanuni ya Kufuta Mabano.

3.3 Hitimisho

Sura hii imebainisha sababu za baadhi za nomino ambatani kukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ilhali zingine hazikiuki kwa kuongozwa na mhimili wa KKM na Kanuni ya Mzunguko Kamili. Sababu za baadhi za nomino ambatani kukiuka KKM zilizojadiliwa katika sura hii ni: mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana na mofu ya kwanza. Mtafiti alibaini kuwa, kuonekana kwa mofu ya pili na mofu ya kwanza husababishwa na: upatanisho wa kisarufi, mgongano wa kiidadi hasa mofu ya kwanza inapochukua kiambishi cha wingi ilhali mofu ya pili haichukui, na mvuto unaotokea hasa nomino ambatani inapoambishwa kisarufi katika hali ya wingi. Pia ilibainika kuwa nomino ambatani hizi hukiuka KKM kutokana na muktadha wa matumizi yake. Kwa upande wa nomino zisizokiuka KKM mtafiti alibaini sababu zifuatazo: mofu ya pili ya nomino ambatani kuwa na mofu kapa, na uundaji wa kimofolojia wa nomino ambatani usiopachika kiambishi cha wingi katika mofu ya pili ya neno husika, yaani mazoea ya kutopachika viambishi vya wingi katika nomino zilizo katika mofu za pili za nomino ambatani hizi. Sura ya Nne inayofuata imeshughulika na kueleza mchango wa ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano kwa wanaleksikografia wa Kiswahili.

SURA YA NNE

MCHANGO WA UKIUKAJI WA KANUNI YA KUFUTA MABANO

4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu utafiti umeshughulikia sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka Kanuni ya Kufuta Mabano ilhali zingine hazikiuki. Mtafiti ameeleza sababu za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ambazo ni: mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana na mofu ya kwanza, na muktadha wa matumizi ya nomino ambatani. Kwa upande wa nomino ambatani zisizokiuka KKM, mtafiti amebaini pia sababu ambazo ni: mofu ya pili ya nomino ambatani kuonekana kuwa na mofu kapa, na uundaji wa kimofolojia wa nomino ambatani usiopachika kiambishi cha wingi katika mofu ya pili.

Sura hii imeshughulikia mchango wa ukiukaji wa KKM ya Mofolojia Leksia kwa wanaleksikografia wa Kiswahili ambao ni: kueleza dhima ya shadda katika nomino ambatani, kuonesha uhusiano wa fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia katika uundaji wa nomino ambatani, na kutofautisha utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili kwa kuongozwa na mhimili wa KKM na Kanuni ya Mzunguko Kamili .Data iliyochanganuliwa katika sura hii, imeorodheshwa katika Viambatisho A na B.

4.1 Kueleza Dhima ya Shadda katika Nomino Ambatani

Kutokana na uchanganuzi wa data kutoka *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015), mtafiti alitumia nomino ambatani sita yaani, tatu zinazokiuka KKM na tatu zisizokiuka KKM kama viwakilishi vya nomino zote sitini kueleza namna ukiukaji wa KKM huchangia kueleza dhima ya shadda katika nomino ambatani. Kulingana na Betti & Ulaiwi

(2018), shadda ni nguvu ya pumzi ambayo hutumiwa kutamkia silabi. Kutokana na fasili hii tunaweza kusema kuwa shadda ni mkazo unaowekwa katika silabi ya neno ili kusikika kwa nguvu zaidi kuliko silabi zingine katika neno linapotamkwa (Mwendamseke, 2017; Massamba, 2011). Jedwali 4.1 lifuatalo linadhihirisha nomino ambatani ambazo zimepachikwa kipambasauti, shadda.

Jedwali 4.1: Uwekaji wa Shadda katika Nomino Ambatani za Kiswahili

Uwekaji wa Shadda kila Neno	**Uwekaji Upya wa shadda**
/mwa'limu m'kuu → mwa'limu m'kuu/	mwalimu m'kuu
/'mwenye 'kiti → 'mwenye'kiti/	mwenye'kiti
/'mke 'mwenza → 'mke'mwenza/	mke'mwenza
/msu'meno 'uta → msu'meno'uta/	msumeno'uta
/kifu'ngua 'mimba → kifu'ngua'mimba/	kifungua'mimba
/'mwendo 'kasi → 'mwendo'kasi	mwendo'kasi

Nomino ambatani za Jedwali 4.1 zinadhihirisha namna kipambasauti shadda hufanya kazi katika mchakato wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili. Ukiukaji wa KKM huwapa wanaleksikografia maarifa ya kuelewa mchakato wa uondoaji wa shadda ya msingi kutoka mofu ya kwanza na uwekaji upya wa shadda ya msingi katika mofu ya pili ya nomino ambatani. Mtafiti alitumia nomino ambatani ‘mwalimu mkuu’ kama kiwakilishi cha nomino ambatani katika Jedwali 4.1 kueleza namna shadda msingi huondolewa na kupachikwa upya katika mchakato wa Fonolojia Mzunguko. Kama ilivyokwisha kudhihirishwa katika Sura ya Pili, maneno haya yakiwa katika hatua ya kwanza kabla kuunganishwa huwa na shadda ya msingi yaani, *mwa'limu* na *m'kuu*.

Katika mchakato uundaji wa nomino ambatani huwa maneno yote yana shadda msingi yaani, *mwa'limu m'kuu* na mabano hufutwa kuashiria mwisho wa ngazi husika ya mzunguko wa fonolojia. Hatua ya mwisho huruhusu shadda ya msingi kuondolewa kutoka mofu ya kwanza ‘mwalimu’ na kupachikwa upya katika mofu ya pili ‘mkuu’

kuwa *mwalimu 'mkuu*. Kinachotokea hapa ni kile Betti & Ulaiwi (2018) wanadai kuwa kila neno huwa na shadda moja ya kimsingi kwa kuelekezwa na mofolojia ya neno husika. Wanachosema Betti & Ulaiwi (keshatajwa) ni kuwa iwapo mofolojia ya neno itakuwa sahili, ambatani au changamani bado shadda ya msingi huwa moja.

Uondoaji wa shadda ya msingi kutoka mofu ya kwanza na upachikaji upya wa shadda ya msingi katika mofu ya pili au tatu ya nomino ambatani huwapa wanaleksikografia maarifa ya kutambua kuwa, kwa kiasi fulani mofu ya kwanza ya nomino ambatani huwa imebakia na mkazo, lakini mkazo huo huwa si mkazo msingi bali huwa wa pili au tatu kutegemea muundo wa nomino ambatani husika na hili hurahisisha mchakato wa upachikaji wa shadda katika nomino ambatani za Kiswahili (Massamba, 2011).

Uondoaji na upachikaji upya wa shadda hautokei katika lugha ya Kiswahili pekee, bali pia unajitokeza katika lugha ya Kihispania na Kiingereza ambapo shadda huondolewa kutoka neno la kwanza na kupachikwa upya katika neno la pili au tatu na zaidi kutegemea mofolojia ya nomino ambatani (Halle, Harris & Vergnaud, 1991). Vilevile, ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano hudhihirisha namna vipambasauti toni na kiinitoni hufanya kazi katika lugha zingine, yaani Kikuria na Kijapani (Odden, 2019; Poser, 1990). Mathalan, uondoaji wa toni katika vitenzi vya Kikuria kutoka kiambishi na kuwekwa upya katika shina la kitenzi, huwapa wanaleksikografia uelewa wa namna vitenzi vya Kikuria vinavyoundwa na kutamkwa kwa ufasaha. Pia ukiukaji wa KKM husaidia kueleza namna kiinitoni hupotea katika nomino zinazoundwa kutoka kwa vitenzi vya Kijapani. Kupotea kwa kiinitoni katika nomino zinazoundwa kutoka vitenzi vya Kijapani ni njia mojawapo ya kuwawezesha wanaleksikografia kuelewa kuwa kila lugha huwa na mchakato maalum wa uundaji

maneno na vipambasauti vya lugha yaani, shadda, toni na kiinitoni hufanya kazi mbalimbali katika uundaji wa maneno ya lugha husika.

4.2 Kuonesha Uhusiano wa Fonolojia, Mofolojia, Sintaksia na Semantiki

Kutokana na uchanganuzi wa data iliyochanganuliwa, nomino ambatani za Kiswahili zilizodhihirisha ukiukaji wa KKM huonesha uhusiano wa fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia ni kama zifuatazo katika Jedwali 4.2 lifuatalo:

Jedwali 4.2: Uhusiano wa Fonolojia, Mofolojia, Semantiki na Sintaksia

Mabadiliko ya Kifonolojia	**Nomino Ambatani Umoja**	**Nomino Ambatani Wingi**
{mu + jomba} → mjomba	[M [kaza**m**jomba]]	[wa [kaza**wa**jomba]]
{mu + tazamaji} → mtazamaji	[M [sikilizaji **m**tazamaji]]	[wa [sikilizaji **wa**tazamaji]]
{mu + zito} → mzito	[M [ja**m**zito]]	[wa [ja**wa**zito]]
{mu + ana} → mwana	[M [kaza**mw**ana]]	[wa [kaza**w**ana]]
{mu + enza} → mwenza	[M [ke**mw**enza]]	[wa [ke**w**enza]]
{mu + enzio} → mwenzio	[M [kuu**mw**enzio]]	[wa [kuu**w**enzio]]
{mu + falme} → mfalme	[**Mw** [ana**m**falme]]	[w [ana**wa**falme]]

Jedwali 4.2 linadhihirisha mabadiliko ya kifonolojia yaani, kudondoshwa kwa irabu /u/ ikitanguliwa na konsonanti, na badiliko la vokali kuwa nusu vokali. Kama ilivyokwisha elezwa katika Sehemu ya 2.3, matawi ya fonolojia na mofolojia huwa na uhusiano katika uundaji wa maneno. Mathalan, nomino ambatani *{mu + kaza} + {mu + {jomba} → mkazamjomba* na *{mu + kuu} + {mu +enzio} → mkuu mwenzio* zinaonesha mabadiliko ya kifonolojia ambapo nomino ambatani ‘mkazamjomba’ imepitia badiliko la kudondosha irabu ikitanguliwa na konsonanti, na mofu ya pili ya nomino ambatani ‘mkuu mwenzio,’yaani, ‘mwenzio’ imepitia badiliko la kifonolojia la vokali kuwa nusu vokali.

Kutokana na mabadiliko haya, ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano husaidia wanaleksikografia kutambua jinsi kanuni za kifonolojia na kanuni za kimofolojia hushirikiana katika uundaji na uambishaji kisarufi wa nomino ambatani za Kiswahili hasa mofu za kwanza na za pili zinapochukua viambishi vya wingi, kinyume na KKM ambayo hairuhusu mofu za pili au tatu katika nomino ambatani kuchukua viambishi vya wingi. Hali hii hueleza jinsi viambishi vya mofu za kwanza katika nomino ambatani za Kiswahili huathiri viambishi vya mofu za pili katika mchakato wa kuziambisha katika hali ya wingi. Maoni haya yanaoana na ya Mpiranya (2015) na Habwe & Karanja (2004) ambao wasema kuwa kiambishi cha kwanza cha nomino ndicho huamua ngeli ya neno na viambishi vya wingi vya nomino husika.

Mtafiti anakubaliana na wataalam hawa, kwa kuwa mabadiliko ya viambishi vya mofu za kwanza katika nomino ambatani za Jedwali 4.2 zinadhihirisha sifa hii, wakati zinapoambishwa katika hali ya wingi na hivyo basi, kuonesha namna Ukiukaji wa KKM una mchango ambao si haba katika kuambisha kisarufi nomino ambatani za Kiswahili. Pia kutokana na mabadiliko haya ya kifonolojia, ukiukaji wa KKM huwasaidia wanaleksikografia kubaini kuwa fonolojia huhusika zaidi na uambishaji kisarufi wa nomino ambatani za Kiswahili kuliko uundaji wa nomino ambatani kwa vile uambishaji huhusisha mofimu za kisarufi na uundaji wa nomino ambatani ukihusisha uunganishaji wa maneno kamili.

Maoni ya Mpiranya (2015) na Habwe & Karanja (2004) yanaoana na yale ya Kiparsky (1982) ambaye anasema kuwa kanuni za kifonolojia na kanuni za kimofolojia hushirikiana katika uundaji na uambishaji kisarufi wa nomino ambatani na katika muktadha wa utafiti huu, ni namna fonolojia na mofolojia hushirikiana katika uambishaji wa nomino ambatani za Kiswahili katika hali ya wingi. Mtafiti

anachoeleza hapa ni kuwa, matawi haya; yaani fonolojia na mofolojia hufanya kazi kwa kushirikiana na hili hubainika kupitia ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano ili kuzalisha maumbo yenye maana kisarufi na kubalifu katika lugha husika. Kiparsky (keshatajwa) anadai kuwepo kwa uhusiano baina ya mofolojia na sintaksia katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili. Anaendelea kusema kuwa miundo ya kisintaksia hufichama ndani ya nomino ambatani hasa zinapotumiwa katika miktadha mbalimbali.

Ukiukaji wa KKM hudhihirisha uhusiano wa mofolojia na sintaksia kupitia nomino ambatani kama vile ‘mwanamfalme,’ nomino ambayo inapoambishwa katika hali ya wingi huwa ‘wanawafalme’ na hili huweka wazi namna miundo ya kisintaksia hufichama katika nomino ambatani hii, hasa inapotegemea muktadha wa matumizi yake. Maarifa haya yatawafaa wanaleksikografia kuunda na kuchanganua aina za nomino zenye sifa hii za kutegemea muktadha wa matumizi yake na hivyo basi kuunda nomino ambatani zilizo kubalifu katika lugha husika.

Kutokana na uwekaji wazi wa mofolojia ya ndani ya nomino ambatani hizi kwa fonolojia, wanaleksikografia wanapata kuelewa namna tawi la semantiki na sintaksia hufanya kazi katika mchakato wa uundaji wa nomino ambatani. Kulingana na Kanuni ya Kufuta Mabano, fonolojia hairuhusiwi kuangalia mofolojia ya ndani ya neno baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa, hali ambayo ni kinyume na nomino ambatani zilizoorodheshwa katika Sura ya Pili ambazo zinaruhusu fonolojia kuangalia muundo wa ndani wa neno hasa zinapoambishwa katika hali ya wingi. Nomino ambatani ambazo mtafiti alibaini zinakiuka Kanuni ya Kufuta Mabano zilizingatia tawi la semantiki na sintaksia ili kuwepo na neno lililo sahihi kisarufi. Tawi la semantiki na sintaksia katika uundaji wa nomino ambatani huhakikisha kuwa maumbo tokeo

hayana uendelezaji wa kisarufi wenye makosa yaani, hutoa mgongano wa kiidadi na huhakikisha upatanisho wa kisarufi ulio sahihi na hii ndiyo sababu nomino ambatani zinazokiuka KKM zilichukua viambishi vya wingi katika mofu za kwanza na za pili ili kuzalisha maumbo-unde yaliyo na maana kubalifu; mathalan, nomino ambatani *mkuu mwenzio → wakuu wenzio* na *baba mkubwa → baba wakubwa*.

Müller (2015) aneleza kuwa katika mchakato wa uundaji maneno, mofimu za maneno hazijifungi katika mofosintaksia pekee bali hujumuisha matawi mengine ya isimu yaani, fonolojia na mofolojia. Maoni haya yanaoana na ya Mashauri (2018) ambaye anasema kuwa, kuwepo kwa uhusiano baina ya matawi ya isimu; mofolojia, fonolojia na semantiki katika mchakato wa uundaji wa nomino ambatani na kuziambisha katika hali ya wingi. Wanachosema Müller (2015) na Mashauri (2018) ni kile mtafiti alirejelea katika utafiti huu kuwa, ufanyaji kazi kikoa wa matawi ya isimu yaani, fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia katika uundaji na uambishaji wa nomino ambata za Kiswahili. Ukiukaji wa KKM huonyesha uhusiano na ufanyaji kazi kikoa wa matawi haya, na hili husaidia wanaleksikografia kuunda nomino ambatani ambazo hazina makosa ya kisarufi kama vile nomino ambatani ‘wakuu wenzio,’ na hili hufanikisha uundaji wa maneno sahihi.

4.3 Kutofautisha Utaratibu wa Uundaji wa Nomino Ambatani za Kiswahili

Data ya nomino ambatani sitini zilizochanganuliwa katika utafiti huu, zilisaidia mtafiti katika kueleza namna ukiukaji wa KKM huwafaa wanaleksikografia wa Kiswahili. Kuonesha namna ukiukaji wa KKM husaidia wanaleksikografia kutambua utofauti uliopo baina ya utaratibu wa uundaji nomino ambatani hizi na namna zinavyochukua viambishi vya wingi zinapoambishwa katika hali ya wingi, utaratibu

wa kila kundi la nomino ulielezwa, yaani utaratibu wa nomino zinazokiuka KKM na zisizokiuka KKM.

4.3.1 Utaratibu wa Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM

Nomino zinazodhihirisha aina ya utaratibu huu, ni nomino ambatani thelathini. Hata hivyo katika sura hii, nomino ambatani tano pekee zilitumiwa kama viwakilishi vya nomino ambatani zingine katika kundi hili. Jedwali 4.3 lifuatalo linadokeza utaratibu wa nomino ambatani zinazokiuka KKM kama ifuatavyo:

Jedwali 4.3: Utaratibu wa Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM

Nomino Ambatani (Umoja)	**Nomino Ambatani (Wingi)**
[**Mw** [enye**ki**ti]]	[**w** [enye**vi**ti]]
[**Ø** [Neno kuu]]	[**ma** [neno **ma**kuu]]
[**M** [kuu **mw**enzio]]	[**wa** [kuu **w**enzio]]
[**Ø** [raia **mw**ema]]	[**ø** [raia **w**ema]]
[**Mw** [ana**m**falme]]	[**w** [ana**wa**falme]]

Kinachodhihirika katika Jedwali 4.3 ni hali ambapo ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano huonesha namna nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM huchukua utaratibu [wingi + Y_1] [wingi + Y_n] katika mchakato wa kuambisha nomino ambatani hizi katika hali ya wingi. Mathalan, kama inavyojitokeza katika nomino ambatani ‘mwenyekiti’ ambapo mofu ya kwanza na pili huchukua viambishi vya wingi kuwa ‘wenyeviti,’ na hili hutokea katika nomino ambatani zote zilizoorodheshwa katika Jedwali 4.2.

Kutokana na utaratibu huu wa ukiukaji wa KKM, wanaleksikografia hutambua sababu za kutokea kwa mabadiliko katikati ya nomino ambatani hizi baada ya vipashio mbalimbali kuunganishwa; sababu ambazo mtafiti amekwisha jadili katika Sura ya Tatu, yaani kuonekana kwa mofu ya kwanza na mofu ya pili na muktadha wa matumizi wa nomino ambatani za Kiswahili. Maarifa haya yatawasaidia

wanaleksikografia kuondoa mgongano wa kiidadi katika sarufi ya maneno kama vile ***wanamke* kuwa *wanawake* na kutambua namna viambishi vya mofu za kwanza katika nomino ambatani huathiri viambishi ambavyo mofu za pili au tatu huchukua wakati zinapoambishwa katika hali ya wingi (Kula, 2012; Gichuru, 2010). Utaratibu huu pia huonesha wanaleksikografia namna nomino zilizo na mofu kapa kama vile; 'raia mwema' na 'nenokuu' huchukua viambishi vya wingi kuwa 'raia wema' na 'manenomakuu,' hali ambayo inarahisisha uundaji na uambishaji wa kisarufi wa nomino ambatani za aina hii.

4.3.2 Utaratibu wa Nomino Ambatani Zisizokiuka KKM

Nomino ambatani za Kiswahili zisizokiuka KKM ambazo zilichanganuliwa katika utafiti huu ni thelathini. Katika sehemu hii, nomino ambatani tano pekee zilitumiwa kama viwakilishi vya nomino ambatani zote katika kundi hili kudhihirisha utaratibu wa kuambisha nomino hizi katika hali ya wingi kama inavyojitokeza katika Jedwali 4.4 lifuatalo:

4.4: Utaratibu wa Nomino Ambatani Zisizokiuka KKM

Nomino Ambatani (Umoja)	**Nomino Ambatani (Wingi)**
[**Ki** [kosikazi]]	[**vi** [kosikazi]]
[**Ki** [umambuzi]]	[**vi** [umambuzi]]
[**M** [sumenouta]]	[**mi** [sumenouta]]
[**Ø [**spanaboi]]	[**ma** [spanaboi]]
[**Mw** [anamgambo]]	[**w** [anamgambo]]

Jedwali 4.4 linadhihirisha nomino ambatani ambazo huchukua viambishi vya wingi katika mofu za kwanza pekee kwa kuchukua utaratibu ufuatao; [wingi + Y1] + [Y_n]. Mathalan, nomino ambatani 'kikosikazi' huchukua kiambishi cha wingi kuwa 'vikosikazi.' Utaratibu huu hukubaliana na KKM na Kanuni ya Mzunguko Kanili ambapo urejeleaji nyuma hautokei katika neno baada ya viambajengo mbalimbali

kuunganishwa kinyume na nomino ambatani zilizoorodheshwa katika Sehemu ya 4.3.1.

Ukiukaji wa Kufuta Mabano huwapa wanaleksikografia wa Kiswahili maarifa ya kuelewa muundo wa nomino ambatani hizi, na kutambua sababu za mofu za pili za nomino ambatani kama vile: ‘spanaboi’ na ‘mwanamgambo,’ yaani ‘boi’ na ‘mgambo’ kutochukua viambishi vya wingi ilhali katika mazingira ya kawaida huchukua viambishi vya wingi kuwa ‘maboi na ‘migambo.’ Katika Sura ya Tatu, sababu hii ilibainika kuwa ni mazoea ya matumizi ya maneno haya na hivyo basi, hili hufanikisha uambishaji wa kisarufi katika hali ya wingi sahihi na uchanganuzi bora wa nomino ambatani za Kiswahili.

Muundo unaorejelewa hapa ni maneno yanayotumika kuunda nomino ambatani za Kiswahili. Kutokana na utambuzi wa maneno haya, wanaleksikografia hupata kujua namna maneno husika huchukua viambishi vya wingi katika mchakato wa kuambishwa katika hali ya wingi na hili huwasaidia katika kuchambua nomino ambatani zinazodhihirisha sifa ya ukapa katika mofu za pili katika nomino ambatani kama vile; ‘kiinilishe’ kuwa ‘viinilishe.’

Kutokana na taratibu hizi mbili za kuambisha nomino ambatani za Kiswahili yaani [wingi + Y1] + [wingi + Yn] na [Wingi +Y1] [Yn] ni dhahiri kuwa ukiukaji wa KKM una mchango ambao si haba kwa wanaleksikografia, kwa kuwa huwaelekeza kutambua muundo wa nomino ambatani na kutambua namna mofu huchukua viambishi vya wingi wakati vinapoambishwa katika hali ya wingi na hili hufanikisha uundaji wa maneno yenye maana kisarufi.

Pia kupitia taratibu hizi, wanaleksikografia hutatua makosa ya kisarufi yanayosababishwa na Kanuni ya Kufuta Mabano ambayo hairuhusu fonolojia kutazama mofolojia ya ndani ya neno husika katika maumbo kama vile, **wajamzito* na hili huleta uzalishaji wa maumbo kubalifu katika sarufi ya lugha husika.

4.4 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti ameeleza kwa mapana mchango wa ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano kwa wanaleksikografia wa Kiswahili, ambapo mtafiti amebaini mchango ufuatao: ukiukaji wa KKM hueleza namna shadda hufanya kazi katika nomino ambatani za Kiswahili, ambapo ilitambulika kuwa ukiukaji wa KKM huwafaa wanaleksikografia kuelewa namna uondoaji wa shadda ya msingi hutokea katika nomino ambatani za Kiswahili hasa shadda ya msingi ya mofu ya kwanza inapopachikwa upya katika mofu ya pili na pia kueleza sababu za kutokuwa na shadda za msingi mbili katika nomino ambatani za Kiswahili.

Vilevile, sura hii, imeshughulikia namna matawi ya isimu yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki hufanya kazi kikoa kwa kuongozwa na Kanuni ya Mzunguko Kamili. Ilibainika kuwa matawi haya hutegemeana katika mchakato wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili ili kuunda neno linalokubalika kisarufi kwa kuelekezwa na kanuni ya lugha husika, na mwisho mtafiti alibaini kuwa ukiukaji wa KKM huwafaa wanaleksikografia kutofautisha utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani zinazokiuka KKM na zile ambazo hazikiuki KKM. Maarifa kutokana na utofautishaji wa utaratibu wa uundaji wa nomino ambatani hizi, utakuwa ni njia ya kuelewa sababu za nomino ambatani kukiuka na kutokiuka KKM kama ilivyokwisha elezwa katika Sura iliyotangulia. Suya ya Tano inayofuata imeshughulikia muhtasari,

matokeo na mapendekezo ya utafiti. Sura hii kwa uwazi inaeleza kile kilichotokea katika uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.0 Utangulizi

Uchunguzi huu ulikusudia kuchanganua ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili kwa madhumuni ya kueleza namna baadhi za nomino ambatani za Kiswahili hukiuka kanuni hii. Utafiti huu ulikuwa na kariha ya kutaka kujua mambo manne: nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM, maumbo ya nomino ambatani za Kiswahili yanayokiuka KKM, sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki na mchango wa ukiukaji wa KKM ya Mofolojia Leksia kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Madhumuni haya yaliafikiwa kupitia; ufafanuzi wa data uliohusisha matumizi ya majedwali, vielelezo na michoro katika kueleza nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka na zisizokiuka KKM. Sura hii imeshughulikia muhtasari, matokeo na mapendekezo ya uchunguzi.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Sura ya Kwanza imeshughulikia kiini cha utafiti na hatua zilizofuatwa katika kujibu maswali ya uchunguzi huu. Uchunguzi huu ulitumia muundo wa kimaelezo katika kuwasilisha matokeo. Utafiti huu ulifanyika maktabani ambapo tasnifu, majarida na makala ya yaliyosakurwa mtandaoni yalitumika. Data iliyochanganuliwa katika uchunguzi huu ilidondolewa kutoka *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) kwa kuongozwa na mbinu ya upekuzi wa yaliyomo ambapo nomino ambatani sitini yaani, thelathini zinazokiuka KKM na thelathini zisizokiuka KKM zilitumiwa kuthibitisha ukiukaji wa KKM. Uchunguzi huu ulitumia nadharia ya Mofolojia Leksia yake Kiparsky (1982)

ambapo mihimili miwili ilitumika katika uchanganuzi wa data, yaani Kanuni ya Kufuta Mabano, na Kanuni ya Mzunguko Kamili.

Sura ya Pili imeshughulikia nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM na maumbo ya nomino ambatani yanayokiuka KKM. Sura hii ilinuia kueleza utaratibu ambao nomino ambatani hufuata katika mchakato wa kuambisha nomino ambatani katika hali ya wingi, mathalan [Wingi + Y_1] + [wingi + Y_n] utaratibu ambao ni kinyume na Kanuni ya Kufuta Mabano ambayo inaruhusu mabadiliko kutokea katika mofu za kwanza pekee kwa kuchukua utaratibu [Wingi + Y_1] + [Y_n]. Pia sura hii ilishughulikia uhusiano uliopo baina ya tawi la mofolojia na fonolojia ambapo ilibainika kuwa matawi haya hutegemeana katika mchakato wa uundaji nomino ambatani na hata katika kuambisha nomino ambatani za Kiswahili katika hali ya wingi. Vilevile, sura hii ilieleza namna shadda hupachikwa katika nomino ambatani za Kiswahili hasa inapoondolewa kutoka mofu ya kwanza na kupachikwa upya katika mofu ya pili au tatu kutegemea muundo wa nomino ambatani husika. Vilevile, mtafiti alibaini nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM kuwa na maumbo mawili kwa kuongozwa na maneno yanayaohusika katika ujenzi wao, yaani nomino ambatani sahili na changamani. Mhimili wa Kanuni ya Kufuta Mabano ulitumika katika sura hii kueleza utaratibu unaohusika katika uundaji wa nomino ambatani hasa kwa kusisitiza kuwa fonolojia haina uwezo wa kuangalia umbo la ndani la neno. Kutokana na mhimili huu ndipo data lengwa ya utafiti huu zilipatakana, yaani nomino ambatani zinazokiuka KKM. Aidha, Kanuni ya Mzunguko Kamili ilitumika kueleza namna shadda huondolewa katika mofu ya kwanza na kupachikwa upya katika nomino ambatani za Kiswahili. Pia mhimili huu ulitumika kueleza uhusiano wa fonolojia na mofolojia katika mchakato mzima wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili.

Sura ya Tatu imeshughulikia sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki. Aidha, imedhihirisha sababu za nomino ambatani kukiuka KKM hasa zinapochukua viambishi vya wingi katika mofu za kwanza na za pili katika mchakato wa kuziambisha katika hali ya wingi. Vilevile, upande wa nomino ambatani zisizokiuka KKM, sababu za nomino ambatani hizi kuonekana kutokiuka KKM zilijadiliwa. Mhimili wa Kanuni ya Kufuta Mabano ulitumiwa kueleza jinsi maumbo ya ndani ya nomino ambatani huwa wazi kwa fonolojia ilhali maumbo ya nomino ambatani zingine hayaonekani na fonolojia. Vilevile, Kanuni ya Mzunguko ya Kamili ilitumikizwakwa kuonesha kuwa katika mchakato wa mzunguko kaida hutawala kila daraja mpaka neno kubalifu kuundwa kabla ya kupitishwa kwa daraja inayofuata. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini baadhi za nomino kukiuka na kutokiuka kaida hizi wakati zinapoambishwa katika hali ya wingi.

Sura ya Nne imeshughulikia mchango wa ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Katika sura hii mtafiti alieleza jinsi ukiukaji wa KKM huwafaa wanaleksikografia kujua dhima ya shadda katika nomino ambatani za Kiswahili. Vilevile, sura hii ilishughulikia namna matawi ya isimu yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki hushirikiana katika mchakato wa uundaji na uambishaji wa nomino ambatani za Kiswahili na kutofautisha utaratibu unaohusika katika kuambisha nomino ambatani za Kiswahili katika hali ya wingi na katika muktadha wa utafiti huu nomino ambatani zinazokiuka na zile zisizokiuka KKM. Mihimili ya Kanuni ya Kufuta Mabano na Kanuni ya Ngazi Leksia ilitumikizwa katika sura hii kueleza namna ukiukaji wa KKM huwa na mchango kwa wanaleksikografia wa Kiswahili.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti alibaini nomino ambatani thelathini za Kiswahili zinazokiuka KKM ambazo zilidhihirisha urejeleaji nyuma katika neno baada ya viambajengo mbalimbali kuunganishwa. Kulingana na KKM, mabano ya mwisho yafutwapo huashiria mwisho wa uundaji wa neno na huruhusu urejeleaji nyuma kutokea katika muundo wa nje wa neno husika pekee. Hata hivyo, hali hii haitokei katika nomino ambatani zote kwa kuwa baadhi za nomino ambatani za Kiswahili hukubali fonolojia kurejelea muundo wa ndani wa neno hasa zinapochukua viambishi vya wingi katika mofu za kwanza na za pili. Vilevile, mtafiti alibaini uwepo wa nadharia inayoweka wazi mofolojia ya ndani ya neno kwa fonolojia yaani, nadharia ya Umbo Upeo (Prince & Smolensky, 1993). Kutokana na nadharia hii ya Umbo Upeo mtafiti alitambua kiini cha nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM kuwa ni kuzalisha maumbo yenye maana kisarufi.

Pia mtafiti alieleza namna upachikaji wa shadda katika nomino ambatani za Kiswahili hutokea, ambapo alibaini kwamba shadda huondolewa kutoka mofu ya kwanza na kupachikwa upya katika mofu ya pili au tatu kutegemea muundo wa nomino ambatani husika. Mihimili ya Kanuni ya Mzunguko Kamili na KKM Ilitumikizwa kueleza daraja ambapo shadda hupachikwa katika mzunguko wa uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili.

Mtafiti alitambua kuwa uondoaji wa shadda ya msingi katika mofu ya kwanza ya neno na kuwekwa upya katika mofu ya pili ya neno husika hudhihirisha kuwa hakuna ukiukaji wa KKM kwa sababu sheria huona hili kama neno moja, si mawili kama awali. Urejeleaji wa muundo wa ndani wa nomino ambatani ni kinyume na KKM ambayo hairuhusu urejeleaji nyuma katika neno baada ya vipashio mbalimbali

kuundwa. Kutoa mwanga zaidi kuhusu namna nomino ambatani za Kiswahili hukiuka KKM, mtafiti aliainisha nomino ambatani husika katika makundi mawili; nomino ambatani sahili na changamani kwa kuongozwa na mihimili miwili; Kanuni ya Kufuta Mabano na Kanuni ya Mzunguko Kamili. Kutokana na makundi haya, maumbo yaliyohusika katika nomino ambatani hizi na kanuni zilizotumika ili kuunda neno kubalifu yalielezwa na mtafiti.

Katika Sura ya Tatu mtafiti alibaini sababu za baadhi za nomino ambatani kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki KKM. Mtafiti alitambua kuwa sababu za nomino ambatani kukiuka KKM ni; kuonekana kwa mofu ya kwanza ya nomino ambatani na mofu ya pili. Kuonekana kwa mofu ya kwanza na mofu ya pili ya nomino ambatani hutokea kutokana na haja ya kuleta upatanisho wa kisarufi, na kuondoa mgongano wa kiidadi unaotokea katika kuambisha nomino ambatani za Kiswahili katika hali ya wingi.

Upatanisho wa kisarufi na mgongano wa kiidadi uliorejelewa hapa ni pale ambapo nomino ambatani zinapoambishwa katika hali ya wingi kwa kuongozwa na KKM huzua nomino ambatani zisizo sahihi kisarufi. Nomino ambatani hizi zilidhihirisha kutokuwa na upatanisho wa kisarufi sahihi kutokana na kuwa na mgongano wa kiidadi yaani, mofu za kwanza zilirejelea wingi ilhali mofu za pili zikirejelea hali ya umoja. Kuondoa hali hii, mofu za pili za nomino ambatani hizi zilichukua viambishi vya wingi ili kuunda neno lililo na maana kubalifu katika sarufi ya Kiswahili. Pia mtafiti alibaini kuwa mofu za pili za baadhi za nomino ambatani huonekana na mofu ya kwanza kutokana na mvutano unaotokea wakati nomino hizi zinapoambishwa katika hali ya wingi. Mvutano katika hali ya wingi unaorejelewa hapa ni mofu za kwanza

kuathiri mofu za pili kuchukua viambishi vya hali ya wingi katika nomino ambatani husika.

Sababu ya pili ya nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ambayo mtafiti alibaini ni muktadha wa matumizi ya nomino ambatani za Kiswahili. Baadhi za nomino ambatani zilidhihirisha kutegemea muktadha wa matumizi yake ndiposa kuchukua viambishi vya wingi katika mofu za kwanza na za pili. Hivyo basi, nomino ambatani hizi, zinaporejelea zaidi ya mtu mmoja huwa kunatokea utata wa kimatumizi na kuondoa utata huu Kanuni ya Kufuta Mabano hukiukwa ili kuunda nomino ambatani zinazotegemea muktadha husika. Ukiukaji KKM uliodhihirika hapa uliingiliana na maoni ya Jeffers & Lehiste (1979) ambao wanadai kuwa maana ya neno hutambuliwa kutokana na seti ya miktadha ambayo neno hilo hutokea.

Kwa upande wa nomino ambatani zisizokiuka KKM, mtafiti alitambua sababu za nomino ambatani hizi kuonekana kutokiuka KKM ambazo ni mofu ya pili ya nomino ambatani kuwa na mofu kapa. Kutokana na uchanganuzi wa data, mtafiti alibaini nomino ishirini na tatu zilizodhihirisha sifa hii. Mtafiti alizigawa katika makundi ya ngeli nne zinamopatikana, yaani ngeli ya A-WA (nomino ambatani saba), ngeli ya KI-VI (nomino ambatani tano), ngeli ya LI-YA (nomino ambatani sita), na ngeli ya U-I (nomino ambatani tano) na kwa kuwa mtafiti alibaini sifa ya ukapa kuwepo katika nomino ambatani hizi, aliteua nomino mbili kutoka kila kikundi kama viwakilishi vya nomino jumla ishirini na tatu. Mtafiti alitambua kuwa sababu za nomino ambatani kutokiuka KKM, ilitokana na mofu za pili za nomino ambatani hizi kuwa na mofu kapa, yaani nomino ambazo katika mazingira ya kawaida hazichukui viambishi vya wingi. Maneno katika mofu ya pili kutokuchukua viambishi vya wingi ni kile Carstens

(1991) anaeleza kuwa kila kundi la nomino huwa linahusishwa na kiambishi fulani cha ngeli na muundo tofauti wa makubaliano yanayozalisha neno kubalifu.

Pili mtafiti alibaini sababu nyingine ya nomino ambatani kutokiuka KKM kuwa uundaji wa kimofolojia wa nomino ambatani usiopachika kiambishi cha wingi katika mofu ya pili. Kinachobainika hapa ni upatanisho wa idadi ambapo nomino ambatani husika hazichukui viambishi vya wingi wakati zinapoambishwa katika hali ya wingi ingawa katika mazingira ya kawaida zilionekana kuchukua viambishi vya wingi. Mtafiti alitambua kuwa mofu za pili za nomino ambatani zisizokiuka KKM hukosa kuchukua viambishi vya wingi kutokana na mazoea ya matumizi yao katika mazungumzo ya kila siku.

Katika Sura ya Nne mtafiti alibaini kuwa ukiukaji wa KKM una mchango kwa wanaleksikografia wa Kiswahili. Kutokana na uchanganuzi wa data ya utafiti huu, mtafiti alitambua kuwa ukiukaji wa KKM huwafaa wanaleksikografia kuelewa dhima ya shadda katika mchakato wa uondoaji wa shadda ya msingi kutoka mofu ya kwanza na uwekaji upya wa shadda ya msingi katika mofu ya pili ya nomino ambatani. Pia mtafiti alibaini kuwa uondoaji wa shadda kutoka mofu ya kwanza na upachikaji upya wa shadda katika mofu ya pili au tatu ya nomino ambatani huwapa wanaleksikografia maarifa ya kutambua kuwa, kwa kiasi fulani mofu ya kwanza ya nomino ambatani huwa imebakia na mkazo, lakini mkazo huo huwa si mkazo msingi bali huwa wa pili au tatu kutegemea umbo la nomino ambatani husika na hili hurahisisha mchakato wa upachikaji wa shadda katika nomino ambatani za Kiswahili (Massamba, 2011).

Pia mtafiti alibaini mchango mwingine wa ukiukaji wa KKM kuwa ni kuonesha uhusiano wa matawi ya isimu yaani, fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia.

Kutokana na mabadiliko ya kifonolojia yaani kudondoshwa kwa irabu inapotanguliwa na konsonanti na badiliko la vokali kuwa nusu vokali, mtafiti alitambua jinsi kanuni za kifonolojia na kanuni za kimofolojia hushirikiana katika uundaji na uambishaji kisarufi wa nomino ambatani za Kiswahili hasa mofu za kwanza na za pili zinapochukua viambishi vya wingi, kinyume na KKM ambayo hairuhusu mofu za pili au za tatu katika nomino ambatani kuchukua viambishi vya wingi. Pia mtafiti alitambua kuwepo kwa uhusiano kati ya mofolojia na sintaksia katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili ambapo mtafiti alibaini miundo ya kisintaksia kufichama ndani ya nomino ambatani hasa zinapotumiwa katika miktadha mbalimbali.

Vilevile, mtafiti alibaini kuwa tawi la semantiki na sintaksia katika uundaji wa nomino ambatani huhakikisha kuwa maumbo tokeo hayana uendelezaji wa kisarufi wenye makosa yaani, hutoa mgongano wa kiidadi na huhakikisha upatanisho wa kisarufi ulio sahihi na hii ndiyo sababu nomino ambatani zinazokiuka KKM zilichukua viambishi vya wingi katika mofu za kwanza na za pili ili kuzalisha maumbo-unde yaliyo na maana kubalifu.

Mchango wa ukiukaji wa KKM uliobainishwa na mtafiti ni, kutofautisha utaratibu wa kuambisha nomino ambatani zinazokiuka KKM na zisizokiuka KKM hasa zinapoambishwa katika hali ya wingi. Kutokana na uchanganuzi wa data, mtafiti alibaini nomino ambatani zisizokiuka KKM kuwa na utaratibu ufuatao [wingi + Y1] + [Y_n] na zile zinazokiuka KKM kuwa na utaratibu [wingi + Y1] + [wingi + Yn] na [Wingi +Y1] [Yn]. Mtafiti alitambua kuwa maarifa kutokana na taratibu hizi mbili za kuambisha nomino ambatani katika hali za wingi yatawafaa wanaleksikografia kuunda nomino ambatani zilizo sahihi na zinazokubalika katika sarufi ya lugha

husika. Kutokana na muhtasari huu, ni wazi kuwa utafiti huu, uliafikia maswali ya utafiti kwa kuwa malengo yote yaliyoongoza utafiti huu yameshughulikiwa katika sura zote nne.

5.3 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili, aina za maneno kama vile vivumishi, vitenzi, viunganishi, viwakilishi na vielezi havikushughulikiwa. Pia utafiti huu ulikumbana na tafiti chache mno zilizoshughulikia ukiukaji wa KKM hivyo basi, kuna haja ya kuwa na tafiti zaidi zinazolenga sehemu hii. Utafiti huu pia ulishughulikia ukiukaji wa KKM katika nomino ambatani za Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksia. Kuna haja ya tafiti kufanywa kuhusu ukiukaji wa KKM katika nomino ambatani kwa kuzingatia nadharia nyinginezo ili kuzalisha maarifa zaidi. Pia kuna haja ya utafiti kuhusu uhusiano wa matawi ya isimu yaani, fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki katika mchakato wa uundaji wa maneno.

Fauka ya hayo, mtafiti alikumbana na changamoto katika uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo kwa kuwa tafiti zilizoshughulikia Kanuni ya Kufuta Mabano hazikuweka wazi dhana ya ukiukaji wa kanuni hii, mtafiti alitatizika katika utumikizi wa mihimili ya nadharia ya Mofolojia Leksia iliyotumika katika utafiti huu na ili kuafikia malengo yote ya utafiti ilimlazimu mtafiti kuongeza lengo la utafiti na hata kuonesha mchango wa ukiukaji wa KKM kwa wanaleksikografia wa Kiswahili na hivyo basi malengo yote ya utafiti huu yaliafikiwa. Ni matumaini ya mtafiti kuwa utafiti huu utakuwa ni kichocheo cha tafiti zaidi.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu umeshughulikia ukiukaji wa KKM katika uundaji wa nomino ambatani za Kiswahili. Nomino ambatani za Kiswahili zinazokiuka KKM na maumbo yake yakielezwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya ML hasa zinapoambishwa katika hali ya wingi. Aidha utafiti huu umechanganua sababu za baadhi za nomino ambatani za Kiswahili kukiuka KKM ilhali zingine hazikiuki, na mwisho mchango wa ukiukaji wa KKM kwa wanaleksikografia wa Kiswahili umetolewa.

Marejeleo

Allen, M. R. (1978). *Morphological Investigations* (Unpublished Doctoral Dissertation). University of Connecticut, Storrs, CT.

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Press.

Benczes, R. (2006). *Creative Compounding in English*. Amsterdam and Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.

Betti, M. J., & Ulaiwi, W. A. (2018). Stress in English and Arabic: A Contrastive Study. *English Language and Literature Studies*, *8*(1), 83-91.

Bisetto, A., & Scalise, S. (2005). The Classification of Compounds. *Lingue e linguaggio*, *4*(2), 319-0.

Booij, G. (1997). Non- Derivational Phonology Meets Lexical Phonology. In I. Roca (ed.), *Derivations and Constraits in Phonology*. Oxford: ClarendonPress, 266-288.

Booij, G. (2014). The Phonology-Morphology Interface. In *The First Glot International State-of-the-Article Book*, 287-306.

Buberwa, A. (2011a). Muundo wa Majina ya Mahali katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Vituo vya Daladala Jijini Dar es Salaam. *Kioo cha Lugha*, *9*(1),1-14.

Buberwa, A. (2011b). Viambishi-ngeli katika Nomino za Pekee: Mifano kutoka katika Majina ya Mahali katika Kihaya. *Kiswahili*, 74(1).

Buberwa, A. (2017). Ruwaza za Kimofolojia za Majina ya Mahali ya Kihaya: Mtazamo wa Mofolojia Leksika. *Kiswahili*, *77*(1).

Carstens, V. M. (1991). *The Morphology and Syntax of Determiner Phrases in Kiswahili* (Published Doctoral Dissertation). University of California, Los Angeles.

Chomsky, N., & Halle, M. (1968). *The Sound Pattern of English*. New York: Harper & Row, Publishers.

Cole, J. (1995). Eliminating Cyclicity as a Source of Complexity in Phonology. In Cole, J., Green. G., & James, M. (eds.), *Linguistics and Computation*. Stanford: CSLI, 255-280.

Creswell, J. W. (2007). *Educational Research Planning and Evaluation: Qualitative and Quantitative Research* (2 ed). Ohio: Prentice Hall, Inc.

Deda, N. (2015). The Phenomenon of Ambiguity in English Language Communication. An Analysis from the Pragmatic Point of View. *Folia Linguistica et Litteraria*, (10), 79-86.

Gichuru, T. M. (2010). *Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksia* (Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Gituru, M. W. (2019). *Unyambulishaji wa Vitenzi Katika Kigĩchũgũ* (Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Chuka.

Habwe, J. H., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Halle, M., Harris, J. W., & Vergnaud, J. R. (1991). A Reexamination of the Stress Erasure Convention and Spanish Stress. *Linguistic Inquiry*, *22*(1), 141-159.

Hammond, M. (1991). Morphemic Circumscription. In Geert Booij and Jaap van Marle (eds.), *Yearbook of Morphology*. Dordrecht: Kluwer. 195-209.

Haspelmath, M., & Sims, A. D. (2013). *Understanding Morphology*. New York: Routledge.

Inkelas, S. (1990). *Prosodic Constituency in the Lexicon*. New York:

Jeffers, G., R. & Lehiste, I. (1979). *Principles and Methods for Historical Linguistics*. Cambridge: MIT Press.

Kahigi, K., K. (2007). Ujanibishaji wa Office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu. *Kioo cha Lugha, 5*(1).

Katamba, F., & Stonham, J. (2019). *Morphology*. New York: Palgrave.

Katikiro, E. G. (2018). Tathmini ya Maana katika Maneno Ambatani ya Kiswahili. *Mulika Journal*, *36*(1).

Kiparsky, P. (1982). 'From Cyclic to Lexical Phonology' in Verder Hulst and Smith (eds).*The Structure of Phological Representation*. Dordrecht: Foris Publication.

Kombe, L. E. (2016). Uambatishaji wa Vishazi katika Lugha ya Kiswahili: Uchunguzi wa Madai ya De Vos na Riedel (2017). *Kioo cha Lugha, 16*(1).

Kothari, C. R. (2004) *Research Methodology: Methods and Techniques* (2rd ed). New Delhi: New Age International Publishers.

Kula, N. C. (2012). Nominal Compounding and Associative Phrases in Bemba. In *Proceedings of the 6th World Congress of African Linguistics* (pp. 431 441).

Longhorn (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publisher.

Lusekelo, A. (2019). Endocentric and Exocentric Compounds in Kiswahili. *SKASE Journal of Theoretical Linguistics*, *16*(4).

Mashauri, M. A. (2018). The Interface Between Morphology, Phonology and Semantics in Standard Swahili Compound Nouns. *Utafiti*, *13*(2), 1-22.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TATAKI.

Mathews, P. H. (1974). *Morphology*. New York: Cambridge University Press.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha na Isimu na Nadharia. Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mcmahon, A. (2000) *Lexical Phonology and History of English.* Cambridge: Cambridge University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu. Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Milroy, A. L. (1987). *Observing and Analysing Natural Languages*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Mohanan, K. P. (1986). *The Theory of Lexical Phonology*. Dordrecht: Reidel.

Mpiranya, F. (2015). *Swahili Grammar and Workbook*. New York: Routledge.

Mugenda, O. M & Mugenda, A. G. (2019). *Research Methods*. *Quantitative and Quantitative Approaches.* Nairobi: ACTS Press.

Müller, P. O. (2015). 45. Rules, Patterns and Schemata in Word-Formation. In Müller, P., Ohnheiser, I., Olsen, S. & Rainer, F. (Ed.), *Volume 2 Word Formation* (pp. 803-821). Berlin, Boston: De Gruyter Mouton. https://doi.org/10.1515/9783110246278-001.

Mustafa, S. K. (2020). Categorization of Compound Nouns in Kurdish and English. *LLT Journal: A Journal on Language and Language Teaching*, *23*(1), 104-115.

Mwendamseke, F., J. (2017). Uamilifu wa Mkazo katika Kiswahili Sanifu. *Mulika Journal*, *35*(1).

Odden, D. (2019). Predicting Tone in Kikuria. *Publications in African Languages and Linguistics*, 311–326. doi:10.1515/9783110882681-02.

Orgun, C. O., & Inkelas, S. (2002). Reconsidering Bracket Erasure. In *Yearbook of Morphology 2001* (pp. 115-146).

Pesetsky, D. (1979). Russian Morphology and Lexical Theory. *Manuscript, MIT*.

Poser, W. J. (1990). The Phonetics and Phonology of Tone and Intonation in Japanese. *Journal of Japanese Linguistics*, *12*(1), 208-209.

Prince, A., & Smolensky, P. (1993). *Optimality Theory: Constraint Interaction in Generative Grammar* (Unpublished, Ms). Rutgers University.

Rasim, T. (2020, November 21). The Triangle of Morphology, Phonology, and Lexicon. Retrieved from https://www.google.com/search?q=The+Triangle+f+Morphology%2C+Phonology+an+Lexicon&oq=The+Triangle+of+Morhology%2C+Phonology+and+Lexicon+&aqs=come..69i57j69i60l3.160j7&srceid=chrome&ie=UTF-8 on 7/04/2021; 12:26PM.

Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Selkirk, E. O. (1982). The Syntax of Words. *Linguistic Inquiry Monographs Cambridge, Mass*, (7).

Siegel, D. (1974). *Topics in English Morphology* (Unpublished Doctoral Dissertation). MIT, Cambridge, Massachusetts.

Tarasova, E. (2013). *Some New Insights into the Semantics of English N+N Compounds* (Unpublished Doctoral Dissertation). Victoria University of Wellington.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

VIAMBATISHO

Kiambatisho A: Nomino Ambatani Zinazokiuka KKM

Nomino Ambatani (Umoja)	Nomino Ambatani (Wingi)
1. [**Mw** [ana**m**ke]]	[**wa** [ana**wa**ke]]
2. [**M** [ja**m**zito]]	[**wa** [ja**wa**zito]]
3. [**Ø [**raia **mw**ema]]	[**ø** [raia **w**ema]]
4. [**Mw** [alimu **m**kuu]]	[**w** [alimu **wa**kuu]]
5. [**Mw** [enye**ki**ti]]	[**w** [enye**vi**ti]]
6. [**M** [ke**mw**enza]]	[**wa**] [ke**we**nza]]
7. [**Mw** [ana**m**kaidi]]	[**w** [ana**wa**kaidi]]
8. [**M** [kaza**mw**ana]]	[**w** [akaza**wa**na]]
9. [**Mw** [ana**m**falme]]	[**w** [ana**wa**falme]]
10. [**Mw** [ana**m**potevu]]	[**w** [ana**wa**potevu]]
11. [**Ki** [rai **k**ielezi]]	[**vi** [rai **v**ielezi]]
12. [**Ki** [rai **k**itenzi]]	[**vi** [rai **v**itenzi]
13. [**Ki** [rai **k**iunganishi]]	[**vi** [rai **v**iunganishi]]
14. [**Ki** [rai **k**ivumishi]]	[**vi** [rai **vi**unganishi]]
15. [**M** [kaza**m**jomba]]	[**wa** [kaza**w**ajomba]]
16. [**Ki** [unga**mw**ana]]	[**vi** [unga**w**ana]]
17. [**M** [kuu **mw**enzio]]	[**wa** [kuu **we**nzio]]
18. [**Mw** [ana**m**kendege]]	[**wa** [ana**w**akendege]]
19. [**Mw** [ana**mw**ali]]	[**w** [ana**wa**li]]
20. [**Mw** [anawa**mw**ana]]	[**w [**anawa**wa**na]]
21. [**Ø** [baba **m**dogo]]	[**ø** [baba **wa**dogo]]
22. [**Ø** [baba **m**kubwa]]	[**ø** [baba **wa**kubwa]]
23. [**Ø** [bwan a**m**dogo]]	[**ø** [bwana **wa**dogo]]
24. [**Ø** [neno**k**uu]]	[**ma** [neno**ma**kuu]]
25. [**M** [hariri **m**kuu]]	[**wa** [hariri **wa**kuu]]
26. [**Ki** [takasa **m**kono]]	[**vi** [takasa **mi**kono]]
27. [**M** [sikilizaji mtazamaji]]	[**wa** [sikilizaji **wa**tazamaji]]
28. [**M** [saidizi mshauri]]	[**wa** [saidizi **wa**shauri]]
29. [**M** [tunga**m**ziki]]	[**wa** [tunga**mi**ziki]]
30. [**Ø** [utiwa**m**gongo]	[**ø** [utiwa**mi**gongo]]

Kiambatisho B: Nomino Ambatani Zisizokiuka KKM

Nomino Ambatani (Umoja)	Nomino Ambatani (Wingi)
1. [**M** [nadiswala]]	[**wa** [nadiswala]]
2. [**Ø** [golikipa]]	[**ma** [golikipa]]
3. [**Ki** [funguamimba]]	[**vi** [funguamimba]]
4. [**Ki** [tindamimba]]	[**vi** [tindamimba]]
5. [**Ki** [chwamaji]]	[**vi** [chwamaji]]
6. [**Mw** [anamgambo]]	[**w** [anamgambo]]
7. [**Mw** [anasiasa]]	[**w** [anasiasa]]
8. [**Ø** [spanaboi]]	[**ma** [spanaboi]]
9. [**Ki** [banuaulimi]]	[**vi** [banuaulimi]]
10. [**Ch** [amshakinywa]	[**vi** [amshakinywa]]
11. [**Ki** [ambajengo]]	[**vi** [ambajengo]]
12. [**Ki** [inilishe]]	[**vi** [inilishe]]
13. [**Ki** [kosikazi]]	[**vi** [kosikazi]]
14. [**Ki** [sengeretua]]	[**vi** [sengeretua]]
15. [**Ki** [pandesauti]]	[**vi** [pandesauti]]
16. [**Ki** [zuianoki]]	[**vi** [zuianoki]]
17. [**Ø** [anguotete]]	[**ma** [anguotete]]
18. [**Ø** [boyaokozi]]	[**ma** [boyaokozi]]
19. [**Ø** [fupanyonga]]	[**ma** [fupanyonga]]
20. [**Ø** [kundishinikizi]]	[**ma** [kundishinikizi]]
21. [**Ki** [umambuzi]	[**vi** [umambuzi]]
22. [**Ø** [punguzobei]]	[**ma** [punguzobei]]
23. [**Ø** [tundadamu]]	[**ma** [tundadamu]]
24. [**M** [fumojike]]	[**mi** [fumojike]]
25. [**M** [kundenyika]]	[**mi** [kundenyika]]
26. [**M** [pilipilitao]]	[**mi** [pilipilitao]]
27. [**M** [sumemouta]]	[**mi** [sumenouta]]
28. [**M** [taimbokombo]]	[**mi** [taimbokombo]]
29. [**M** [tambaapanya]]	[**mi** [tambaapanya]]
30. [**Mw** [endokasi]]	[**mi** [endokasi]]

Kiambatisho C: Vibali ya Utafiti

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 22nd April, 2021

TO: Ayiega Mofart Onyoni
C/o Kiswahili & African Languages Dept.

REF: C50/28000/2018

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 18th November, 2020 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, "Ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika Uundaji wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksia".

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

HARRIET ISABOKE
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Daktari Chacha Mwita
C/o Department of Kiswahili & African Languages
Kenyatta University

HI/lnn

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

Our Ref: C50/28000/2018

DATE: 22nd April, 2021

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR AYIEGA MOFART ONYONI - REG. NO. C50/28000/2018.

I write to introduce Ayiega Mofart Onyoni who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the Department of Kiswahili & African Languages.

Ayiega intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, "Ukiukaji wa Kanuni ya Kufuta Mabano katika Uundaji wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksia".

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

PROF. ELISHIBA KIMANI
AG. DEAN, GRADUATE SCHOOL

HI/bm